




**Dk.** Mwinyi: Bila utawala wa sheria hakuna maendeleo

UKURASA 3




## RAPHINHA: NILIPOTEZA MARAFIKI KWA UHALIFU

UKURASA 21


# Nipashe JUMAPILI


**Jumapili Septemba 18, 2022** • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581072

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

### MTAALAMU AONYA...

# Unywaji huu wa pombe ni hatari kiafya

• **Ataja** kiwango kinachokubalika kwa wanaume na wanawake, aanika dalili mbaya... *Endelea ukurasa 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa Askofu Mkuu Mstaafu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, John Ramadhan, jana katika Kanisa Kuu la Mkunazini, Dayosisi ya Zanzibar, Mkunazini. Maziko ya kiongozi huyo yalifanyika katika viwanja vya kanisa hilo, Mjini Unguja. **PICHA: IKULU.**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 5**

**MBARONI TUHUMA WIZI WA NG'OMBE, PUNDA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Ruvuma linawashikilia wafugaji 10 kwa tuhuma za wizi...

**UKURASA WA 8**

**WATAKA MUSWADA SHERIA YA NDOA UWASILISHWE BUNGENI**

UMOJA wa Wanawake Wanaotetea Wanawake na Wasichana Tanzania (TAPO)...

## Auawa kikatili kisa miguu ya ng'ombe

UKURASA 8

### RIPOTI MAALUM

## Mtoto aliyefungiwa ndani alivyonajisiwa, kupata VVU

UKURASA 4

**MICHEZO** **SIMBA, BIG BULLETS HAPATOSHI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Vigogo CWT wapigwa 'stop'

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Chama cha Walimu Tanzania (CWT), limewasimamisha katika nafasi zao za uongozi na utendaji aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama hicho, Deus Seif na Mweka Hazina, Abubakary Allawi.

Viongozi hao waliokuwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 39 ya mwaka 2021, walikutwa na hatia ya jinai ya matumizi mabaya ya madaraka na uchepushaji wa fedha za CWT, Sh. 13,930,963 walizochukua kwa ajili ya kwenda kuangalia mpira wa miguu Cape Verde.

Vilevile, wawili hao walihukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kifungo cha miezi sita na kutakiwa kurejesha fedha zote walizochukua.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Rais wa CWT, Dina Mathamani, alisema viongozi hao wamesimamishwa katika kikao cha dharura cha Baraza la Taifa kilichofanyika juzi na jana kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali likiwamo suala hilo.

Kaimu Rais alisema baada ya viongozi hao kukutwa na tuhuma hizo, ziliwasilishwa kwenye kikao cha baraza ambacho ndicho chombo chenye mamlaka ya kuchukua hatua kwa viongozi wa chama.

"Moja ya masuala yaliyojadiliwa na Baraza la Taifa ni hukumu dhidi ya viongozi wakuu wa Chama cha Walimu Tanzania, ambao aliyekuwa Katibu Mkuu, Mwalimu Deus Seif na aliyekuwa Mweka Hazina wa CWT Taifa, Abubakar Salum Allawi," alisema.

Mathamani, alisema viongozi hao wanaoendelea na adhabu ya kutumikia kifungo cha miezi sita, walikutwa na hatia katika kesi ya uhujumu uchumi namba 39 ya mwaka 2021 ya jinai ya matumizi mabaya ya madaraka na uchepushaji wa fedha za CWT, Sh. million 13.9 ambazo wametakiwa kuzirejesha baada ya kumaliza adhabu yao.

Kaimu Rais huyo alisema baraza hilo limewasimamisha nafasi zao za uongozi na utendaji ndani ya Chama cha Walimu Tanzania, wakisubiria uamuzi wa mkutano mkuu wa taifa unaotarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu.

"Baraza limekutana na kuamua kuwasimaisha kwa mujibu wa Katiba ya CWT, ambayo inaelekeza moja ya adhabu ni kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya viongozi wa kitaifa ambao wanachaguliwa na mkutano mkuu endapo tu watakwenda kinyume," alisema Mathamani.

Pia alisema, adhabu zilizopo ni pamoja na kuwaonya na kuwasimamisha uongozi wakati wakisubiri uamuzi wa mkutano mkuu wa taifa ambao utatoa mapendekezo kama kuwasamehe au kuwapa adhabu zaidi.

Alifafanua kuwa katika kipindi chote hicho, watu hao watakuwa wamesimamishwa na hawatajishughulisha na kitu chochote ambacho kinahusu Chama cha Walimu Tanzania.

Akizungumzia kuhusu kikao hicho ca Baraza la Taifa, Mathamani alisema kimehudhuriwa na wajumbe wasiopungua 200, ambao walijadili na kutoa uamuzi huo kwa mujibu wa Katiba ya CWT.

"Kikao cha Baraza cha Dharura kimefuata taratibu zote na hii imekuja baada ya viongozi hao kukutwa na tuhuma hizo zilizosababishwa wao kuhukumiwa kifungo cha miezi sita jela," alisema Mathamani.

Aliongeza kuwa, mkutano mkuu wa mwaka unatarajiwa kuhudhuriwa na wajumbe wasiopungua 1,000 kutoka mikoa mbalimbali.

■**Imeandaliwa na Renatha Msungu na Paul Mabeja**



Ofisa Miradi wa Asasi ya kiraia ya Health Integrated Multisectoral Development (HIMD), Wendi Brenda, akifafanua kwa waandishi wa habari kuhusu aina za ukeketaji zinazofanywa katika jamii za kifugaji ambazo bado zinafanya tohara kwa wanawake, walipoitembelea asasi hiyo, katika Halmashauri ya Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mtaalamu: Unywaji huu pombe ni hatari

**Na Mary Geofrey**

UNYWAJI wa pombe zaidi ya kiwango kilichopangwa imezoeleka kuwa jambo la kawaida kwa watumiaji wengi wa kilevi hicho kwa kuamini wanamudu kiasi cha unywaji bila kupata madhara yoyote.

Dhana hiyo inapingwa vikali na Mratibu wa Kituo cha Kitaifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Yohana Goshashy, akiweka wazi madhara ya sumu zitokanazo na pombe ni makubwa licha ya watu wengi kutoyatambua.

Amesema kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, sumu ya pombe inaongoza kwa kusababisha vifo vya watu wengi ikifuatwa na sumu ya kung'atwa na nyoka.

Alisema kwa mujibu wa watafiti, asilimia 75 ya wanywaji wa pombe nchini hufika hatua ya kupata sumu mwilini itokanayo na kilevi.

Goshashy alibainisha hayo katika mazungumzo na Nipashe wiki hii kuhusu madhara ya sumu ya pombe.

Alisema sumu ya pombe inawekwa kwenye kundi la sumu za vyakula kwa kuwa ni kitu mtu anatumia kwa lengo la kujiburudisha.

Alisema ili mtu atumie kwa usalama kuna kiwango cha kutumia ili asipate madhara ya sumu ya pombe na anapaswa kunywa kwa kiwango kilichoshauriwa na wataalamu.

Goshashy alisema viwango vya unywaji vinatofautiana kati ya mwanaume na mwanamke, hivyo mwanaume anaweza kunywa uniti mbili sawa na mililita 600 hadi 700 kwa siku, sawa na chupa mbili za bia.

Alifafanua kuwa mwanamke anatakiwa anywe mililita 300 hadi 350 kwa siku, hivyo hapaswi kuzidisha ili asipate sumu itokanayo na pombe.

Alisema mtumiaji anayekunywa divai, anatakiwa kupunguza kiwango kwa sababu ina kilevi kikali zaidi asilimia 10.

Goshashy alisema divai (wine) yenye kilevi cha asilimia saba, hivyo mtumiaji anatakiwa kunywa nusu glasi, sawa na bia mbili.

Alisema anayekunywa pombe kali, anatakiwa kunywa mililita 15 hadi 20 kwa siku kwa kuwa zina kiwango kikubwa cha kilevi, hivyo anapaswa kuwa na hadhari kuepuka sumu ya pombe.

"Lakini utashangaa kuna watu wanachukua chupa ya pombe kali na kumaliza yote, wapo wanaomaliza kreti zima la bia. Mtu wa aina hii amepanda daraja ya ulevi na yupo kwenye hatua ya 'addiction' (uraibu), hali ambayo inaufanya mwili wake uweze kumudu sumu," alisema.

Alifafanua zaidi kuwa, mtu wa aina hiyo huanza taratibu kuongeza kiwango cha unywaji hadi kufikia hatua hiyo ya kiwango cha juu.

"Tena unakuta watu kama hawa wanajisifu hata ninywe pombe kiasi gani siwezi kulewa, mtu wa aina hii anakuwa ameshapata sumu nyingi mwilini hadi kuwa 'addicted' (kuwa mraibu) na pombe," alisema.

**MBINU ZA KUKWEPA**

Mtaalamu huyo wa sumu alishauri kuwa ili kuepuka sumu ya pombe, unatakiwa kula chakula cha kutosha cha jamii ya wanga.

Alisema chakula cha wanga husaidia kuongeza sukari mwilini na sumu ya pombe husababisha kushusha sukari ya mwilini, hivyo hudhibiti madhara hayo.

"Mtu akijua anataka kunywa, ale vyakula vya wanga kwa kiasi kikubwa ili unavyokunywa usipate madhara ya sumu ya pombe. Ndiyo sababu wengine huwa wanakula nyama wakati wakiwa wanakunywa pombe, hii ni kwa sababu nyama ina wanga," alisema.

Alifafanua kuwa ukiacha shughuli za kawaida kama kutembea, kazi kubwa inayofanywa na ubongo ni kufikiri na hivyo anayekunywa pombe nyingi na kupata sumu, humfanya uwezo wake wa kufikiri kupungua.

Alisema kuwa ili kuepuka madhara, mtumiaji wa pombe anatakiwa kuchanganya kilevi chake na maji au kinywaji kingine kisicho na kilevi ili kupunguza sumu ya pombe.

**MADHARA KIAFYA**

Goshashy alisema madhara makubwa ya kunywa pombe nyingi ni kuchanganyikiwa, kushindwa kufikiri sawasawa na kushindwa kujidhibiti, kushindwa kusimama mwenyewe, kuishiwa nguvu na joto la mwili kushuka.

Alitaja madhara mengine ni kukandamiza sehemu za ubongo ambao unadhibiti sehemu nyingi za mwili na hivyo kusababisha mtu kujisaidia haja ndogo mara kwa mara na hivyo mwili kupoteza maji mengi.

"Ukiona mnywaji anakwenda kujisaidia haja ndogo mara kwa mara, tambua kuwa kashapata sumu ya pombe mwilini na anapunguza kiwango kikubwa cha maji na baadhi ya madini kwa njia ya mkojo," alisema Goshashy.

Aliyataja madini anayopoteza mnywaji wa pombe ni Calcium na Sodium ambayo husaidia kudhibiti mapigo ya moyo na mwisho husababisha madhara makubwa zaidi.

Alisema madhara mengine ni kuta za tumbo kuchubuka na pombe kali zinazosababisha sumu mwilini.

Alibainisha kuwa aliyepata sumu mwilini, atashindwa kumeza vizuri chakula na kumeng'enywa vyema tumboni.

Alisema madhara mengine ni ini kuzungukwa na mafuta mengi na kusababisha kuharibu mfumo wa kongosho.

Goshashy alisema sumu ya pombe pia inaharibu mfumo wa mlalaji na kumkosesha mnywaji usingizi kutokana na kuingilia mfumo wa kudhibiti usingizi.

Alisema athari nyingine ni mtu kushindwa kuacha kunywa pombe na kujikuta anakunywa mfululizo na wakati mwingine kushindwa kufanya chochote bila kunywa.

**DALILI ZA HATARI**

Goshashy alisema zipo dalili za hatari ambazo humpata mtu na kumfanya awe katika hatari kubwa ya kupoteza maisha ikiwamo kushindwa kupumua vizuri.

Alisema dalili mojawapo ya mtu ambaye amepata madhara makubwa ya sumu ya pombe ni kutetemeka, joto la mwili kushuka, kuishiwa nguvu na wakati mwingine kupoteza fahamu.

Alisema wengine hubadilika rangi na kuwa bluu, kutapika na wakati mwingine mwingi kupata homa kali.

Goshashy alisema mtu aliyefika hatua hiyo, anapaswa kukimbizwa hospitalini kupata huduma ya matibabu ili kuepuka madhara makubwa zaidi ikiwamo kupoteza maisha.

## HABARI KITAIFA

# Mbunge ahoji ujenzi wa vituo vya afya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema imeshatoa maelekezo kwa halmashauri zote kuweka vipaumbele vyao vya ujenzi wa vituo vya afya katika tarafa na kata za kimkakati.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alibainisha hayo bungeni juzi alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Vwawa mkoani Songwe, Japhet Hasunga.

Katika swali lake, Hasunga alihoji ni lini serikali itaanza kujenga kituo cha afya katika kata za Msia na Ihanda zilizoko jimboni kwake.

Akimjibu mbunge huyo, Dk. Dugange alisema serikali imeshatoa maelekezo kwa halmashauri zote kuweka vipaumbele vyao vya ujenzi katika tarafa na kata za kimkakati.

"Kama hizi ni kata za kimakakati Mheshimiwa Spika, nimhakikishe Mheshimiwa Hasunga kwamba serikali kupitia mapato ya ndani na kupitia fedha za serikali kuu, tutaendelea kuweka hatua za ujenzi ili vituo viweze kukamilika," alisema.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) ulioanza kutekelezwa mwaka 2008, serikali inaelekezwa kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati na kila kata inakuwa na kituo cha afya ili kusogeza huduma za afya kwa wananchi.

Utekelezaji wa mpango huo pia umewekwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa mwaka 2020-2025.



Magari yakiwa yamekwama katika barabara ya Mandela jijini Dar es Salaam jana kutokana na ufinyu wa barabara hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwinyi: Bila utawala wa sheria hakuna maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mafanikio ya ukuaji wa uchumi, uendeshaji wa biashara, uwekezaji na ustawi wa wananchi yanategemea kuwapo misingi ya utawala wa sheria na uhuru wa mahakama.

Alitoa kauli hiyo jana baada ya kuzindua ripoti ya mahitaji ya mfumo wa mahakama na uzinduzi wa ofisi ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), upande wa Zanzibar, hafla hiyo ilifanyika Hoteli ya Goden Tiliyopo kisiwani hapa.

Alisema, lazima kuwa na sheria madhubuti zinazojenga jamii na kuwa na mifumo bora ambayo lazima iongeze kasi katika kusikiliza na kuamua kesi mahakamani ili haki ipatikane kwa wakati.

Alisema, matumaini yake kuwa mfumo wa mahakama utaimarisha utendaji na kuleta ufanisi kwa kuleta mapinduzi makubwa katika upatikanaji wa haki Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema, serikali yake itaendelea kutoa ushirikiano katika kuhakikisha malengo ya kuanzishwa mfumo huo yanafikiwa.

"Nitaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwamo asasi za kiraia katika kuzipatia ufumbuzi kero na vikwazo vilivyopo katika kuhakikisha mipango yenu inafanikiwa," alisema.

Dk. Mwinyi, alisema uzinduzi wa ripoti hiyo ya mahitaji ya mfumo wa mahakama utaleta mabadiliko yenye lengo la kuwa na Zanzibar yenye uchumi mkubwa na imara na kuleta ustawi bora wa wananchi.

Alisema, hali hiyo itafikiwa kwa kuhakikisha kuendelea kuheshimu sheria na misingi ya haki za binadamu.

Dk, Mwinyi alitoa wito kwa wadau kujielekeza katika kuzingatia na kutekeleza misingi hiyo kwa lengo la kudumisha na kuendeleza amani na misingi ya utawala bora.

Alisema, katika kukabiliana na shida ya miundombinu ya mahakama ripoti hiyo imependekeza kuwapo mpango wa maendeleo ya kimiundombinu na serikali yake iko tayari kushirikiana na wadau katika kufanikisha hilo.

Alisema, jitihada za awali zimeshanza na wanaendelea kuimarisha mazingira ya watumishi wa mahakama, pia kuboresha maslahi yao. Alisema, imani ya wananchi kwa mahakama inachangiwa pia na hali ya watumishi wake katika kuzingatia maadili ya utendaji wa haki.

Hata hivyo, Rais Dk. Mwinyi, alisema vyombo vya sheria vinavyotoa haki, vinalalamikiwa kwa kuwapo baadhi ya watumishi wasiozingatia maadili ya kazi zao, wanajihusisha na rushwa, uzembe, ubadhirifu na kutofuata sheria katika utekelezaji wa majukumu yao. "Vitendo vya aina hii vinakwenda kinyume cha misingi ya utawala bora na vinatia doa katika utendaji wa haki," Rais Dk. Mwinyi alionya.

Aliwataka watumishi wa mahakama kufanya kazi kwa kuzingatia maadili na uadilifu katika utoaji wa haki ili wananchi waendelee kuwaamini.

Alipongeza taasisi hiyo kwa kufungua ofisi zake Zanzibar na ushirikiano inaoutoa kwa serikali ikiwamo kupinga vitendo vya udhalilishaji ambapo serikali yake inaunga mkono jitihada hizo.

Jaji mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdallah, alisema mahakama inakabiliwa na shida nyingi na inashirikiana na asasi za kiraia ikiwamo THRDC kutatua shida hizo. Alisema, mahakama imesimamia nidhamu kwa watendaji wake wakiwamo majaji na mahakimu na kuunda kamati ya nidhamu na maadili inayoshughulikia malalamiko dhidi yao.

Alizitaja baadhi ya shida zinazowakabili ni mrundikano mkubwa wa mashauri na katika kulitatua hilo wameongeza idadi ya majaji na mahakimu ili kutoa uamuzi haraka.

Mratibu wa Kitaifa wa Taasisi ya Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania, Onesmo Olengurumo, alisema asasi za kirai ziko tayari kufanya kazi na serikali katika kutatua kero mbalimbali.

# Wahukumiwa kunyongwa kwa kumuua askari polisi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WATU watano, wakiwamo wanne waliokamatwa kwa tuhuma za kuwaua askari wawili wa Jeshi la Polisi Kituo cha Usoke wilayani Urambo mkoani Tabora, wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kutiwa hatiani na Mahakama Kuu Kanda ya Tabora.

Adhabu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Tabora aliyekasimiwa mamlaka ya ziada, Jovin Katto, baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Waliopewa adhabu hiyo katika kesi ya kwanza ni Shedrack Rushikama, Sylvesta Kingwendu, Abel Benedict na Ramadhani Manywele, waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka mawili ya mauaji na unyanganyi wa kutumia silaha.

Alisema kuwa mahakama pasipo shaka yoyote imewatia hatiani washtakiwa hao baada ya kupata ushahidi usiotia shaka.

Hakimu huyo alisema kutokana na baadhi ya watu kuamua kujichukulia sheria mikononi, adhabu hiyo ni fundisho kwa kila anayetumia nguvu kupora au kuua mtu mwingine.

Upande wa mashtaka uliongozwa na mawakili Meroto Ukongoji na Tunosye Luketa, ukidai mahakamani kuwa watuhumiwa hao walitenda makosa hayo mnamo Aprili 28, 2014 majira ya usiku eneo la Usoke.

Mawakili hao walidai kwamba siku hiyo, washtakiwa walimuua askari polisi mwenye namba G3388 PC Shabani Mbua na namba G 4602 kwa kuwapiga risasi.

Askari hao wawili waliuawa wakati wakitekeleza majukumu yao ya ulinzi na usalama kwenye Kituo cha Polisi Usoke wilayani Urambo mkoani Tabora mwaka 2014.

Akitoa uamuzi huo, Hakimu Katto alisema mahakama imewatia hatiani kwa makosa hayo, hivyo inawahukumu kunyongwa hadi kufa lakini wanaruhusiwa kukata rufani kama hawakuridhika na adhabu hiyo.

Upande wa utetezi katika shauri hilo ulikuwa unawakilishwa na mawakili Flavian Fransisi, Amos Gaise, Christina Jacson na Charles Hayo.

Katika shauri lingine, Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Tabora imemhukumu kunyongwa hadi kufa Nelson Maige baada ya kumtia hatiani kwa kumuua mkewe kwa kutumia kitu chenye ncha kali kutokana na wivu wa mapenzi.

Upande wa mashtaka ulidai mahakamani huko kuwa Oktoba 12, 2019, katika Kijiji cha Loya, Wilaya ya Uyui mkoani hapa, mshtakiwa alimuua mkewe aitwaye Vailet kwa kumchoma kisu shingoni.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DASTUN GABRIEL MSUYA**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 457 AFC** (Toyota hiace) ,Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi au piga simu namba **0718841033/0765841033. DSM/PHQ/ RB/369246/2022.**

RIPOTI MAALUM

# Mtoto aliyefungiwa ndani alivyonajisiwa, apata VVU

Na Romana Mallya



WASWAHILI wanasema 'kweli ni mtihani'. Katika zama za umri mdogo wengi wanakumbuka matunzo bora ya nyumbani yenye usalama, yaliyoendana na kumsimamia mtoto kuhakikisha muda wote anapatikana nyumbani.

Lakini ya leo hii ni mtihani zaidi. Mzazi anajitahidi kumtunza mtoto nyumbani, kinachomfika ni kilio kwao wote, anapomwacha akacheze nje, huko ndiko kuna balaa zaidi.

Rejea sura ya mikasa hii; wazazi wanatengana, mtoto analelewa na baba mdogo na kuishia kulawitiwa na kupata Virusi vya Ukimwi (VVU), bibi anajitahidi kumpeleka mtoto kupata masomo ya ziada (tuisheni) na mtoto huyo anaangukia katika balaa kutoka kwa mwalimu, babu jirani anayepokea shikamoo kila siku, naye anaangukia kwenye dhambi ya hayo hayo.

Mama naye anapigana kumfungia binti yake, anapomaliza sekondari, anapata salamu za mimba mfululizo, huku kuna mama na baba wenzake wana yao kwamba, binti yao aliyeolewa wiki mbili tu, amebakwa na wanaume wanne na historia yake inaonyesha aliwahi kupitia mateso ya aina hiyo akiwa mdogo. Sasa wapi penye nafuu?

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto unaoshughulikia haki ya mtoto kote duniani uliopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1989 na kuridhiwa nchini mwaka 1991, unaelekeza uhuru wa mtoto kuchanganyika na jamii.

Katika mkataba huo kuna tahadhari ya usalama wa kisaikolojia kwa mtoto na hata kukosa fursa yake ya kuchanganyika na kukua kiakili.

### MKASA KAMILI

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Pascal Kisibo, kutoka Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto Kanda Maalum ya Dar es Salaam, anasimulia matukio mawili ya ukatili wa kijinsia ambayo ni miongoni mwa yaliyoripotiwa dawatini mwaka huu, yakihusisha watoto wawili wa kike na wa kiume.

Kisibo anasimulia namna mwanafunzi ambaye mwaka huu alitakiwa kuingia darasa la saba, alivyolawitiwa na baba yake mdogo, aliyekuwa akiishi naye na kuishia kupata maambukizi ya VVU.

Anasema tukio hilo lilitokea mwaka huu wakati mtoto huyo akisoma katika shule ya msingi iliyoko maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam (jina tunalihifadhi).

"Mtoto huyu alikuwa analawitiwa na baba yake mdogo ambaye alimchukua na kukaa naye baada ya wazazi wake kutengana. Wazazi walipotengana, mtoto alibaki na baba lakini kutokana na shida ya malezi kutoka kwa baba na vitendo vya ulevi, alichukuliwa na kwenda kuishi kwa baba yake mdogo," anasema.

Kisibo anasimulia kuwa baba yake mdogo alianza kumlawiti mtoto huyo na kitendo hicho kilifanyika kwa muda mrefu na kusababisha mtoto kuathirika kisaikolojia na kufikia hatua akiwa shuleni wakati wa mapumziko, alikuwa akitoroka na kwenda Bonde la Mto Msimbazi kwa wavuta bangi, ili wamfanyie ukatili huo.

"Taarifa ilipofika kwa walimu wake, hatua zilizochukuliwa, wakati wa mapumziko walikuwa wakimpatia kazi nyingi ili asitoroke. Kilichotokea kutokana na kudhibitiwa, akawa anawaomba watoto wenzake pindi wanapokwenda chooni wamwingilie, wenzake wakawa wanaogopa.

"Ilifikia hatua akawa anajitenga, anakaa peke yake, anachukua peni anajiingiza, mwisho wa siku, walimu wakaligundua kupitia wanafunzi wenzake waliokuwa wakimshuhudia. Mpaka kesi hii inafika dawatini, kwa bahati mbaya mtoto huyu alipopimwa alikutwa tayari ana maambukizi ya VVU," anafafanua.

Kisibo anasema kwa sasa mtoto huyo amehamishiwa kwenye kituo cha kulelea watoto na anaendelea na masomo na mtuhumiwa ambaye ni baba mdogo alishakamatwa.

Tukio la pili linalosimuliwa na Kisibo ni la binti wa kidato cha pili katika shule ya serikali iliyopo Tabata (jina linahifadhiwa), ambaye wakati akiishi na baba yake mzazi na mama wa kambo, mzazi wake alianza kumtaka kimapenzi.

"Kitendo hicho kilimwathiri mtoto kisaikolojia hata katika masomo yake, bahati nzuri mtoto alimshirikisha mama wa jirani na walimu ndipo dawati tukapigiwa simu na kufuatilia tukio hilo na ndipo tulipomwokoa mtoto na sasa anaishi kituo maalum cha malezi ya watoto na mzazi alikamatwa," anasimulia.

### WATOTO KUFUNGIWA

Janet Joseph, mzazi na mkazi wa Mwenge wilayani Kinondoni, akizungumzia kuhusu athari zinazowakuta watoto wanapokuwa nje ya nyumba, anasema ameamua kuchukua hatua ya kuwafungia watoto wake, isipokuwa kwa safari za lazima kama vile shuleni na kanisani, kinyume cha hapo hakuna safari.

Maoni ya mama huyo yanaangukia katika chungu kimoja na mwenzake, Rosemary Haule, anayesisitiza msimamo wa marufuku kwa wanawe kutoka nje ya uzio wa nyumba, akiogopa madhila hayo ya ukatili dhidi ya watoto.

Hata hivyo, Mwanasaikolojia kutoka Hospitali ya Kanda ya Mbeya, Mbuwi Ndagamsu anapinga kitendo cha wazazi kuwafungia watoto, badala yake anawataka wazazi wabebe jukumu la kuhakikisha wanawapatia malezi bora na ulinzi bila kuathiri ukuaji wao wa kila hatua.

"Kumfungia unamjengea mtoto hofu, hataweza kuchangamana na wenzake, hataweza kutambua hisia za wengine, akiwa mkubwa ndiyo anasikia ukatili hata kwenye ndoa, pia watoto hawa huwa wabinafsi.

"Mtoto anapaswa kulindwa na kuelimishwa na afanye mambo kulingana na umri, hatua za ukuaji wake, mzazi anapaswa ahakikishe zinafuatwa bila kurukwa, asije akafika umri fulani akawa anafanya mambo ya umri mdogo na wawekewe misingi ya kujua mema na mabaya, hapa ndipo inaingia dini," anatoa angalizo.

Mwanasaikolojia huyo pia anasema kumfungia mtoto ndani hupunguza uwezo wake wa kufikiri, kunamnyanyapaa na kumnyima haki yake ya kuona thamani ya watu wengine.

Angalizo la mtaalamu huyo wa saikolojia linapata uthibitisho kutoka kwa Caren Mmari, mzazi na mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, anayesimulia kilichojiri kwa mwanawe mwenye umri wa miaka tisa sasa, aliyelelewa kwa mtindo huo wa kufungiwa ndani.

Mama huyo anasimulia kuwa mwanawe huyo anayesoma darasa la tatu jijini, licha ya kuwa na umri huo wa muongo mmoja kasoro mwaka mmoja, anashindwa kutamka vyema baadhi ya maneno ya Kiswahili, jambo lililompa mzazi hofu na kuamua kumpeleka hospitalini.

Anaeleza kuwa alishtuka na kulazimika kuwaona wataalamu wa afya miaka mitano iliyopita baada ya mwanawe huyo kushindwa kabisa kutamka baadhi ya maneno ya Kiswahili, tofauti na wenzake wenye umri wake (kipindi hicho miaka minne) na madaktari walithibitisha hakuwa na tatizo lolote katika mfumo wake wa matamshi.

Anasimulia kuwa ilimchukua muda mrefu kugundua kuwa kinachomrudisha nyuma mtoto wake kuongea vizuri ni kitendo cha kumfungia ndani, bila kuchangamana na watoto wenzake kwa hofu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Shuhuda hizo ni uthitisho kwamba yapo mengi yawapatayo watoto licha ya wazazi kuamini kuwafungia ni mwarobaini wa kutatua tatizo. Je, ni yapi hayo, fuatilia sehemu ya pili ya ripoti hii kesho.

HABARI KITAIFA

## TAMWA yahamasisha uandishi habari za jinsia

**Na Christina Haule**

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, amewataka waandishi wa habari nchini kuandika kwa kina habari kuhusu masuala ya jinsia ili kuifanya jamii kuwa na uelewa mzuri na kupiga hatua katika maendeleo.

Alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam alipowasilisha mada ya dhana ya jinsia wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari kutoka mikoa ya Manyara, Morogoro na Kilimanjaro yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kupitia mradi wa kuleta mabadiliko kwa wanawake wa vijijini (RWCC) unaofadhiliwa na Serikali ya Canada.

Dk. Rose alisema iwapo kutakuwa na uelewa mzuri katika masuala ya jinsia, jamii itaendelea kwa namna mbalimbali ikiwamo kukua kiuchumi na hata kutimiza malengo 17 ya milenia.

"Hata katika malengo ya milenia suala zima la jinsia ni suala mtambuka na linaingia katika kila sekta kwa sababu ndiko kuna watu na linagusa wanawake na wanaume na kama kuna usawa wa jinsia, tunaweza kutimiza malengo yote ya Milenia kuanzia la kwanza hadi la 17," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kumekuwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia wa aina mbalimbali ukiwamo ukatili katika ndoa, jamii, mabadiliko ya tabianchi na maendeleo ya wanawake na uongozi, ambayo yote kwa pamoja yanapaswa kuwekwa wazi na jamii kutambua na kujitambua ili kupiga hatua za maendeleo kama inavyokusudia.

Dk. Rose aliwataka waandishi wa habari kubadilika na kujikita katika kuandika habari za jinsia kwa lengo la kuondoa tatizo na kuleta mabadiliko bila kuacha habari katikati kama vile kuna mtu anakwenda kuimalizia baadaye.

Mratibu wa Mradi wa RWCC, Catherine Kasimbazi, aliwataka viongozi kuanzia ngazi ya wilaya, kata, vijiji na vitongoji sambamba na viongozi wa vituo vya taarifa na maarifa kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari ili kuelimisha jamii juu ya masuala ya kijinsia, hasa ukatili wa kingono.

Akizungumzia mradi wa RWCC, Kasimbazi alisema mradi huo unatekelezwa kwa miaka sita kuanzia mwaka 2021 katika nchi tatu; Tanzania, Kenya na Ethiopia ambapo kwa Tanzania unatekelezwa katika mikoa ya Manyara, Morogoro na Kilimanjaro.

Alisema lengo kuu la mradi huo ni kuleta usawa katika maeneo matatu ambayo ni wanawake na uongozi na ngazi za kufanya uamuzi, ukatili wa kingono (SGBV) na kilimo na mabadiliko ya tabianchi.

Kasimbazi alisema katika utafiti mbalimbali waliofanya kwenye mikoa inayotekeleza mradi, wamebaini kuwapo shida mbalimbali ambazo pia zipo katika mikoa mingine ya Tanzania ikiwamo wanawake kukosa uongozi kwa sababu wanaume kujiona wao pekee ndiyo wenye nafasi na uwezo wa kuwa viongozi.

Alitaja shida zingine ni ukatili wa kingono unajitokeza hata kwenye mabadiliko ya tabianchi ambapo njaa huwa sababu ya kuwapo kwa biashara ya ngono kwa wanawake dhidi ya wanaume, ndoa na mimba za utotoni kufuatia wazazi kuchukua hatua za kuwaozesha mabinti wakiwa katika umri wa mdogo ili wapate pesa, wanawake kujikita kwenye biashara ambazo hazina faida kubwa, rushwa ya ngono, lugha za udhalilishaji wa kingono, matusi, ulawiti na ubakaji.

# Mbaroni tuhuma wizi wa ng'ombe, punda

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

JESHI la Polisi Mkoa wa Ruvuma linawashikilia wafugaji 10 kwa tuhuma za wizi wa ng'ombe 200, punda wawili na kondoo, mali ya James Magese, mkazi wa Kijiji cha Mbatamila wilayani Tunduru.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Marco Chilya, alisema tukio hilo lilitokea Julai 14 mwaka huu nyumbani kwa Magese eneo la Mbatamila.

Alisema baada ya wizi huo kutokea, juhudi za kutafuta zilifanyika bila mafanikio ndipo Magese na wafugaji wenzake walipotoa taarifa polisi Septemba 11 mwaka huu na siku tatu baadaye waliwapata ng'ombe 159 kati ya 200 walioibwa.

Kamanda Chilya alisema kutokana na tukio hilo, wanawashikilia watu 10 wanaodaiwa kuhusika na wizi huo.

Katika tukio lingine, kamanda huyo alisema wanawashikilia watu wengine wawili wanaodaiwa kujihusisha na shughuli haramu za ujangili na biashara ya meno ya ndovu.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Hemed Ally (35), mkazi wa Kijiji cha Mchoteka na Yasini Nyahale (35), mfanyabiashara katika Kijiji cha Chengena wilayani Namtumbo.

Alisema watuhumiwa hao wanashikiliwa baada ya msako kufanyika katika wilaya mbili ya Tunduru na Namtumbo ambapo mtuhumiwa Ally inadaiwa alikutwa na vipande vinne vya meno ya ndovu yenye uzito wa kilogramu 39.45, yakiwa kwenye mifuko miwili ya sandarusi.

"Mtuhumiwa Nyahale, mfanyabiashara wa Namtumbo, alikutwa na nyara za serikali ambayo ni meno mawili ya ndovu, alikuwa yamehifadhiwa nyumbani kwake chini ya kitanda cha watoto wake," alisema.

Kamanda huyo alitaja thamani ya meno yote yaliyokamatwa kuwa ni dola za Marekani 30,000, sawa Sh. milioni 69.499.



Wachuuzi wa mbuzi wakisubiri wateja katika mnada wa Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. Mbuzi mmoja aliuzwa kwa bei ya 80,000/- hadi 120,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maofisa afya wabanwa uchafuzi wa mazingira

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MAOFISA afya mkoani hapa wameagizwa kuzitumia sheria zilizopo kuwachukulia hatua baadhi ya watu wanaochafua mazingira maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini ikiwamo barabara kuu na makaburi.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao kazi cha maofisa afya kutoka halmashauri za Mkoa wa Singida katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Victoria Ludovick.

Alisema serikali inathamini suala la usafi wa mazingira kwa kuwa ndiyo mhimili mkubwa wa afya ya watanzania na ukuaji wa uchumi.

"Tumieni Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 na kanuni zake, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na sheria ndogo za miji kuhakikisha maeneo ndani ya Mkoa wa Singida hayachafuliwi ovyo, ikiwamo barabara kuu, stendi, masoko, mitaro, maeneo ya wazi, makazi na makaburi," aliagiza.

Mwaluko aliagiza maeneo ya masoko na biashara wananchi waweke vyombo vya kuhifadhi taka vyenye ukubwa wa kutosha kulingana na uzalishaji wa taka kwa lengo la kupunguza taka kuzagaa ovyo mitaani.

"Kuna maeneo ambayo tumeona hadi yanarushwa kwenye mitandao, Manispaa (Singida) ndiyo kioo chetu cha Mkoa wa Singida, tuhakikishe usafi unafanyika maeneo yawe safi," aliagiza.

Alisema yapo baadhi ya magari ya abiria yanasimama porini na abiria kuchimba dawa (kujisaidia) vichakani, jambo ambalo halikubariki, hivyo akawaagiza maofisa afya wahakikishe wanachukua hatua.

Mwaluko alisema maofisa afya wa Mkoa wa Singida wanafanya kazi vizuri kutekeleza Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira lakini lazima kuhakikisha fedha inayotolewa na serikali matokeo yake yanaonekana.

Aliongeza kuwa wakurugenzi wa halmashauri, waganga wakuu, maofisa afya na watendaji wa vijiji na kata wasimamie ili kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo bora.

Alisema taarifa zilizopo hadi Julai 31 mwaka huu, kaya zenye vyoo katika Mkoa wa Singida ni asilimia 99.2 na zisizokuwa na vyoo ni asilimia 0.8, zenye vyoo bora ni asilimia 62.1 kutoka asilimia 27.6 mwaka 2015.

"Mimi kama Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, sitavumilia kuona magonjwa ya aibu kama vile kipindupindu yakitokea katika mkoa wangu, hivyo mjipange katika hili," alionya.

Alisema maofisa afya watambue kuwa wao kama wasimamizi na wafuatiliaji wakuu wa shughuli za chanjo, ukaguzi wa dawa, ukaguzi wa vyakula na ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za afya shuleni na taasisi zote, hivyo waongeze bidii kusimamia hayo.

Ofisa Afya Mkoa wa Singida, Mgeta Sebastian, alisema maeneo mengi ya mijini, hata yale ambayo wanapita viongozi wakuu, ni machafu, hivyo wanapaswa kuchukua hatua kuhakikisha wanasimamia ili kuweka mazingira safi.

Sebastian alisema katika suala la usimamizi wa afya atakuwa mkali na ofisa afya asiyetekeleza majukumu yake kama inavyotakiwa, atachukuliwa hatua ikiwamo kutoa taarifa kwa wakuu wake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada za pamoja zitumike kumaliza wimbi la Panya Road

**KATIKA** siku za karibuni, kumekuwa na taarifa za kukithiri kwa vitendo vya kihalifu vinavyofanywa na makundi ya vijana, maarufu kama 'Panya Road'. Vijana hao licha ya kuvamia na kuiba mali katika makazi ya watu na mitaani, wamekuwa wakiwajeruhi na hata kusababisha vifo kwa baadhi ya wananchi.

Licha ya kuibuka hivi karibuni, vitendo hivyo vimekuwa vikijirudia mara kwa mara. Pamoja na kuvamia kwenye makazi ya watu, vijana hao wamekuwa wakivamia magari kwenye foleni wakiwa na silaha za jadi na kupora mali za wananchi na kuwajeruhi baadhi ya watu walioko katika vyombo vya usafiri.

Jeshi la Polisi kwa kiasi kikubwa limekuwa likidhibiti vitendo hivyo ikiwamo kuwachukulia hatua wanaodaiwa kuhusika na vitendo hivyo. Lakini kuibuka kwa wimbi la 'panya road' hivi karibuni, kumeibua minong'ono mwa wananchi na hata baadhi kudhani kwamba jeshi hilo limeshindwa kukabiliana na wimbi hilo ambalo kwa sasa linaonekana kuwa tishio kwa uhai wa raia pamoja na mali zao.

Madai hayo ya wananchi yanatokana na kasi mpya ya vijana hao kuvamia maeneo mbalimbali na kupora, kujeruhi hata kusababisha vifo vya watu. Mfano ni tukio la karibuni lililotokea eneo la Kawe Mzimuni na kusababisha kifo cha mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC). Kutokana na vitendo hivyo kushika kasi, baadhi ya wabunge katika mkutano unaoendelea jijini Dodoma, waliomba mwongozo kwa Spika wa Bunge wakitaka shughuli za Bunge ziahirishwe kwa muda ili kupata wasaa wa kujadili jambo hilo. Hata hivyo, Spika alitoa uamuuzi kwa niaba ya Bunge kwamba serikali ilishughulikie suala hilo ambalo linaonekana kama mfupa mgumu mbele ya vyombo vya usalama.

Kutokana na kuibuka kwa vilio kutoka kwa wananchi pamoja na wabunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, na Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, juzi waliibuka na kutoa kauli nzito kuwaomya Panya Road dhidi ya vitendo hivyo na kwamba siku zao zinahesabika.

Waziri Masauni katika kauli yake, aliwaonya vijana wanaojihusisha na vitendo hivyo vya kihalifu pamoja na kutoa tahadhari kwa watu wanaonunua bidhaa za wizi kutoka kwa Panya Road kuwa watashughulikiwa kikamilifu kwa mujibu wa sheria. Alisema pamoja na nguvu kubwa kutumika kupambana na Panya Road, pia wanaonunua bidhaa zinazopatikana kupitia vitendo hivyo watambue kwamba hawako salama. Hatua ya Waziri na IGP kujitokeza hadharani imeleta matumaini kwa wananchi kwamba kuna hatua ambazo zitachukuliwa na kuwafanya wananchi kuwa katika mikono salama na kuendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo. Matumaini hayo pia yanaonekana baada ya kuwapo taarifa kuwa baadhi ya watuhumiwa katika maeneo mbalimbali, Dar es Salaam , wameaanza kuchukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kutiwa nguvuni.

Pamoja na juhudi zilizoanza kuchukuliwa, ni vyema jitihada zaidi zikachukuliwa dhidi ya watu hao ambao wamekuwa tishio kwa maisha ya raia na mali zao. Viongozi wa serikali za mitaa ambako matukio hayo yamekuwa yakijitokeza, wanapaswa kuchukua hatua kwa kuimarisha ulinzi shiriki na kufanya utambuzi wa vijana wanaojihusisha na matukio hayo ambayo yameanza kulitia doa taifa.

Ni wazi kwamba nguvu ya pamoja, kwa maana ya wananchi kupitia serikali za mitaa kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, itasaidia kutokomeza vitendo hivyo na jamii kuendelea kuishi katika amani na usalama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kukatisha dozi ya ARV ni kujimaliza

**TANGU** ugonjwa wa UKIMWI ulipoingia nchini miongo mitatu iliyopita, juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanyika ili kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama na wale walioambukizwa, wasiusambaze kwa wengine.

Hatua hizo za kupambana na ugonjwa huo zimesaidia kuongeza watu wanaotumia dawa za kufubaza virusi vya ugonjwa huo (ARV) kutoka asilimia 95 ya mwaka 2016 hadi asilimia 98 kwa mwaka 2019.

Takiwmu hizo zinabainishwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, huku akihimiza Watanzania kuendelea kutumia dawa hizo bila kuchoka.

Lakini jambo la msingi analosisitiza ni kuwataka Watanzania kila mmoja kupima kwanza na kwamba akibainika kuwa ameambukizwa, aanze kutumia dawa hizo katika kipindi chote cha maisha yake.

Pamoja na juhudi hizo za kupambana na ugonjwa huo, inaelezwa kuwa kati ya watu 100 wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU), watano hawatumii dawa za kufubaza virusi hivyo, hali inayoonyesha kusuasua kwa utumiaji.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo hivi karibuni alipotembelea zahanati ya Disunyala wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, na kufafanua kuwa asilimia tano ya watu wanaoishi na VVU hawatumii ARV.

kutokana na hali hiyo, iko haja ya Watanzania kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya kuhusu matumizi ya dawa hizo badala ya kuishia njiani hali ambayo wanaeleza kuwa inaweza kuwasababishia matatizo zaidi.

Kama wasemavyo wataalam hao kuwa wakati mwingine mtu anaweza kutumia dawa hizo akajikuta anatapika au kuhara, lakini anatakiwa kutoacha badala yake aendelee kutumia na kwamba hatimaye hali itakuwa vizuri.

Hata wale wanaotumia na kisha CD4 zikapanda na kuonekana wana afya nzuri hawatakiwi kuacha, kirusi hujiimarisha zaidi na kushusha kinga, hali inayoweza kusababisha kupoteza maisha.

**Hata wale wanaotumia na kisha CD4 zikapanda na kuonekana wana afya nzuri hawatakiwi kuacha, kirusi hujiimarisha zaidi na kushusha kinga, hali inayoweza kusababisha kupoteza maisha.**

Umuhimu mwingine unaolekezwa na wataalam wa afya kuhusu matumizi ya dawa hizo ni kuzimeza kwa wakati na sio kubadali saa, kulala kwa wakati, kufanya mazoezi na kupata mlo wa kutosha, kwa ajili ya kuimarisha kinga.

Kwa kuzingatia maelekezo hayo ya wataalam wa afya, ni imani kwamba asilimia ya watumiaji wa dawa za kufubaza virusi hivyo itaendelea kuongezeka, kutoka idadi ya sasa na kuwa juu zaidi.

Kwa sasa inaelezwa kuwa imeongezeka kutoka asilimia 87 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 92 mwaka 2019, lakini inawezekana asilimia hiyo ikaendelea kuongezeka iwapo masharti ya kuzitumia yatazingatiwa.

Lakini kwa njia hiyo, vifo vinavyotokana na Ukimwi vinaweza kupungua zaidi, kwani inaelezwa kuwa tangu mwaka 2010 vimepungua kutoka 64,000 hadi kufikia 32,000 mwaka 2020. Vilevile, inaelezwa kuwa idadi ya maambukizi mapya yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020, hali ambayo ninaamini kuwa iwapo maelekezo yataendelea kuzingatiwa, kuna uwezekano wa kushuka zaidi.

Takwimu za Umoja wa Mataifa zinaonyesha kuwa mwaka 2020, takriban watu milioni 38 duniani kote walikuwa wanaishi na VVU huku 700,000 wakiwa wamefariki dunia kutokana na magonjwa yanayohusiana na Ukimwi.

Hayo ni kwa mujibu wa Shirika la Utangazaji la Uingereza likikariri daktari mmoja liliyemtaja kwa jina la Dk. Kamarulzaman, katika taarifa yake ya Desemba mwaka jana.

Katika mahojiano na watu mbalimbali, ikabainika kuwa baadhi ya vijana huona kama Ukimwi ni ugonjwa wa wazee, ni kitu cha zamani, na kwamba hawana uelewa wa kutosha.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Ijue Jumuiya ya Afrika Mashariki, inavyotenda kazi na vyombo vyake



Pascal Mayalla

KWA Maslahi ya Taifa, inaendelea kuhusu Ijue Jumuiya ya Afrika Mashariki. Leo nikijikita kwenye Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nikiwapeleka sura kwa sura. Sura ya kwanza ni tafsiri tuu maneno, hii nimeiruka na kuanza na sura ya pili.

Sura hii inajumuisha pamoja na uanzishwaji wa jumuiya yenyewe, Ibara ya Pili inahusu uanzishwaji wa Muungano wa Forodha wa Afrika Mashariki na Soko la pamoja. Ibara ya 3 inahusu muundo wa Jumuiya.

Kibali na kutaja nchi tatu za Afrika Mashariki, Tanzania, Kenya na Uganda kama wanachama waanzilishi, imeweka sifa na masharti kwa nchi ziingine kujiunga ni kuubali mkataba, kukubali kanuni za demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu, mchango madhubuti wa nchi inayotaka kuwa mwanachama katika uimarishaji ushirikiano; ujirani mwema, uanzishaji na uendelezaji wa soko huria, na kukubali sera za kiuchumi na kijamii za jumuiya.

Ibara ya 4 inahusu uwezo wa kisheria wa jumuiya. Mbali na kuwa na hadhi ya kuwa chombo cha ùshirikiano, jumuiya itakuwa na uwezo wa kupata, kumiliki, kutumia na kuuza ardhi na mali nyingine. Inaweza kukopa, kushitaki na kushitakiwa pia. Katibu Mkuu ndiye atakayekuwa. mwakilishi wa Jumuiya.

Ibara ya 5, inataja madhumuni ya Jumuiya, ambayo ni pamoja na kuunda sera na pragramu zinazolenga katika kuendeleza ushirikiano katika nyanja za siasa, uchumi, jamii, utamaduni, ulinzi, usalama, sheria na shughuli za mahakama. Katika kutimiza madhumuni haya, nchi wanachama zinakubaliana kuchukua hatua za kuanzisha muungana wa farodha, soko la pamoja, na baadaye, muungano wa sarafu na hatimaye shirikisho la kisiasa.

Ibara ya 6, inahusu misingi muhimu ya Jumuiya, ambayo ni pamoja na amani, upendo, mshikamano, ushirikiano, kuaminiana na ujirani mwema, utatuaji wa migogoro kwa nia ya amani, nchi kufuata misingi ya utawala bora, ugawanaji sawa na kwa haki manufaa ya Jumuiya.

Aidha, Ibara ya 7 inahusu misingi ya utekelezaji ya Jumuiya, ambayo ni pamoja na ushirikiano unaoendeshwa na watu wenyewe kwa utaratibu wa soko huria, uandalizi wa sera zinazovutia na miundombinu bora, uanzishaji wa sera za kiuchumi. zitakazosaidia uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje, kufuata kanuni ya kusaidiana; na ugawanaji wa haki wa faida itokanayo na shughuli za Jumuiya.

Ibara ya 8 inahusu hatua za jumla za utekelezaji.

**UANZISHAJI VYOMBO VYA JUMUIYA**

Ibara ya 9 inahusu uanzishwaji na uundaji wa vyombo na taasisi za jumuiya na idara na vitengo mbalimbali. Kila chombo kina majukumu yake maalum. Vyombo hivi vinapewa uwezo na majukumu kutoka jumuiya yenyewe. Mkutano wa Wakuu wa Nchi unaweza kuanzisha chombo kingine kipya.

Kwa sasa vyombo vya Jumuiya ni saba ambavyo ni Mkutano wa Wakuu wa Nchi, Baraza la Mawaziri, Kamati ya Uratibu, Kamati za Sekta, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Afrika Mashariki na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sura ya nne inazungumzia Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama na inajumuisha Ibara ya 10 mpaka ya 12.

Ibara ya 10 inahusu muundo wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi ikieleza kuwa utawahusisha viongozi ambao ni wakuu wa nchi au wakuu wa serikali za nchi wanachama. Kwa sasa hivi, wakuu hawa ni maraisi wa nchi wanachama, wa nchi zote saba inazounda EAC ambao wanatoka Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Ibara ya 11 na ya 12 zinahusu kazi za Mkutano wa Wakuu wa Nchi kwamba, pamoja na mambo mengine, utakuwa unatoa maelekezo ya jumla kwa jumuiya. Hata hivyo, wakuu hao wa nchi wanaweza kukasimu madaraka yao kwa maofisa au vyombo vingine.

Mkutano wa Wakuu wa Nchi ndio utakaokuwa ukitathmini hali ya amani na usalama katika eneo la Jumuiya. Utaangalia pia, uwezekano wa kusonga mbele katika kuanzisha shirikisho la kisiasa. Pia mkutano huu utakuwa ukiongozwa na mwenyekiti ambaye ni Rais wa mojawapo ya nchi wanachama. Uenyekiti huu utakuwa ukidumu kwa mwaka mmoja mmoja na utakuwa na mzunguko kutoka nchi moja hadi nyingine miongoni mwa nchi wanachama.

Shughuli nyingine zitakazofanywa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi ni pamoja na kuteua Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki, kupokea wanachama wapya, au kukaribisha watazamaji.

**BARAZA LA MAWAZIRI**

Ibara ya 13 inazingatia muundo wa Baraza la Mawaziri. Baraza hili litaundwa na mawaziri ambao watakuwa wameteuliwa tayari na nchi zao kwa malengo ya ushirikiano wa kimataifa au kwa malengo ya ushirikiano wa Jumuiya.

Kadhalika, Ibara ya 14 inahusu kazi za Baraza la Mawaziri ambazo zitakuwa pamoja na kutengeneza sera za jumuiya. Baraza litakuwa pia na kazi ya kuangalia shughuli za kila siku za Jumuiya ikiwa ni pamoja na kukagua na kusimamia shughuli hizo.

Baraza hili ndilo litakalokuwa na jukumu la kuangalia kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea na shughuli zake kama kawaida. Baraza la Mawaziri litakutana mara mbili kwa mwaka.

Wiki Ijayo nitaemdelea kwa Mahakama ya Afrika Mashariki na Bunge la Afrika Mashariki

**Wasalaam**
**Paskali 0754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Tutunge sheria na tuziheshimu bure



Na Joseph Kulangwa

ZAMANI tukiwa wadogo tulipenda sana kwenda kucheza na kuangalia mchezo wa soka viwanjani. Mji tulioishi kulikuwa na uwanja mzuri tu wa soka, kukiwa na mashindano ya klabu za soka.

Moja ya klabu hizo ilikuwa ya Jeshi. Tulipenda sana kwenda kuangalia siku timu hiyo ikicheza na timu nyingine. Tulipenda mechi hizo si kwa sababu ya uzuri wao, bali vituko vya mechi yenyewe.

Daima timu ya Jeshi ilikuwa ikitaka ishinde. Siku ikishindwa mechi haikuwa inafikia tamati, lazima varangati lingeibuka, kama si kwa wachezaji wa timu pinzani kula mkong'oto, basi uliwakuta waamuzi hususan wa kati.

Watoto tulifurahi sana kuona watu wanapigana. Tulipata cha kusimulia nyumbani baada ya kushuhudia wanajeshi wakitembeza mkong'oto kwa wachezaji au waamuzi. Na kwa kweli wanajeshi waliogopwa.

Hao walikuwa wanajeshi wa Jeshi la Wananchi, si wa Polisi, ingawa nao tuliwaogopa hususan wale waliokuwa na magari yenye namba zilizoandikwa FFU (Field Force Unit) lakini tukitafsiriwa kwa Kiswahili kuwa ni kifupi cha Fanya Fujo Uone.

Na kweli watu waliofanya fujo waliona kwani kulikokuwa na fujo yoyote iwe ya kwenye mikusanyiko ya watu au hata kwenye wizi wa mifugo, hao jamaa walipelekwa kufanya kazi. Hakika nao waliogopwa kwa kuwa walitisha. Walitisha hata kwenye magwaride ya sikukuu walivyokuwa wakinyanyua miguu yao na kukanyaga kwa kishindo.

Hakika zamani Jeshi lolote lilikuwa la kuogopwa kwani askari akitoa amri alisikilizwa na mpewa amri alilazimika kutii. Kinyume chake aliona kilichomnyima nyoka miguu. Lakini, baadaye majeshi yalianza kuwa rafiki na raia, ingawa si sana. Ndiyo sababu siku hizi unaweza kusikia kuwa askari hana rafiki, kwani anaweza kukugeuka saa yoyote ukikosa adabu.

Hivi karibuni, kuna jambo lilinishangaza na kwa kweli kila aliyeliona atakuwa alishangaa. Clip ya video ikionesha wafanyakazi wa Kampuni ya Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam (DART) wakikabiliana na askari wa FFU katika moja ya barabara za mabasi ya mwendokasi.

Kinachoonekana pale ni wafanyakazi hao katika barabara hiyo wakizuia gari la askari kupita kwa mujibu wa sheria lakini bahati mbaya walizidiwa na askari hao na gari hilo kuendelea na safari, licha ya mfanyakazi mmoja kujitoa na kujaribu kulizuia kwa mikono.

Shukuru Mungu bila shaka dereva wa lile gari alikuwa muungwana, vinginevyo angemmwaga ubongo yule mfanyakazi wa DART. Hata hivyo, kilichobainika pale ni kwamba askari wale bila shaka walikuwa ama wakienda au wakitoka lindo. Mungu aliepusha maafa.

Naamini wangekuwa wale askari wa enzi zile, wale wafanyakazi wangepata lifti ya bure ndani ya gari lile na kuondoka nao na baadaye wangeapa kutorudi kufanya kazi ile na kuomba mafao yao kabla ya wakati. Lakini bila shaka nidhamu jeshini inarejea.

Hata hivyo, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillius Wambura, aliamua kulitolea kauli lile jambo, akirejea sheria za DRT na matumizi ya barabara zake, akibainisha ni magari gani yanapaswa kutumia njia zile na kwa nini.

Kwa mujibu wa sheria hizo alizozitaja IGP, magari yanayoruhusiwa kupita njia zile ni ya Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, magari maalumu ya kubeba wagonjwa (Ambulance), magari ya fedha hasa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na ya majeshi ya ulinzi na usalama, lakini kwa kibali maalumu cha DART.

Ingawa, kuna mahali alisema hata ya viongozi wa Serikali wanaokuwa wamechelewa na wanaharakisha kwenda mahali fulani-kwa nini lakini wasiwahi? Lakini alisema haya hayo yaliyotajwa hapo awali, lazima yawe na dharura si kupita kwa sababu tu ya kupita.

Hebu turejee ustaarabu kwamba sheria hizo ziliwekwa ili zifuatwe, kwa sababu maalumu, hivyo kuzivunja ni ukaidi ambao hauwezi kuvumiliwa. Tena viongozi na hasa wa Serikali na magari yao ndio wanaopaswa kufuata na kuzingatia sheria zinazotungwa na Bunge, kwa madhumuni mahususi.

Inashangaza kwamba askari polisi wanaokamata madereva wanaovunja sheria katika barabara mbalimbali nje na ndani ya miji na majiji, ndio hao wanaotumia nafasi zao kupita kwenye barabara za mwendokasi na kuvuruga utaratibu wa mabasi ambayo ni mahsusi kawa njia hizo. Tuheshimu sheria na tuheshimiane tufike salama. Alamsiki!

**Baruapepe: kulangwasos@gmail.com**

# Aua kisa miguu ya ng'ombe

**Na Mary Mosha,** SIHA

MKAZI wa Kijiji cha Naibili wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, Safarini Mrema (39), amefariki dunia baada ya kushambuliwa na wananchi maeneo mbalimbali ya mwili wake, ikiwamo kukatwa miguu, wakimtuhumu kukutwa na miguu ya ng'ombe wa jirani yake aliyedaiwa kukatwa miguu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simoni Maigwa, alikiri kutokea kwa tukio hilo Jumatano Septemba 14 mwaka huu na kwamba jeshi hilo linaendelea kufuatilia.

Akisimulia kuhusu tukio hilo, mwanakijiji Lucas Ruben alisema Mrema alishambuliwa na wananchi kwa kucharangwa panga miguu yote na kujeruhiwa mikononi na kichwani.

"Siku ya tukio kijana huyo inadaiwa alimkuta ng'ombe wa jirani yake amefungwa kwenye eneo na shamba lake kwa ajili ya malisho, akamkata miguu ya nyuma na kuondoka nayo kama kitoweo, ili umwonyesha mwenye ng'ombe ambaye ni jirani yake hajapendezwa na kitendo hicho.

Alisimulia kuwa baada ya ng'ombe huyo kupiga kelele, mwenye mfugo wake alipofika eneo la tukio, alimkuta amelala chini bila miguu ya nyuma huku kukiwa na alama za damu zinazoelekea nyumbani kwa Mrema.

"Mwenye ng'ombe alimkuta jirani yake (marehemu) akiwa katika maandalizi ya kitoweo, ndipo alipopiga kelele za kuomba msaada na wananchi wakafika na kumshambulia,"Ruben alisimulia.

Mwanakijiji mwingine James Kimath alisimulia kuwa wakati wa kipigo, mtuhumiwa alipata upenyo na kukimbia, ndipo wananchi walipoamua kubomoa nyumba yake na kuharibu mazao yake shambani, kitendo ambacho kilimfanya arejee nyumbani.

"Wananchi wa kijiji chake walishamchoka, inasemekana ni mtu wa matukio ya wizi na uporaji, kupiga na kunyang'anya, pia alikuwa ni mtumiaji wa dawa za kulevya," Kimath alidai.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Benedict Mallya alisema kijana huyo ametekeleza tukio hilo kwa lengo la kujipatia kitoweo.

"Ni kweli alitekeleza tukio hili na wananchi walipofika nyumbani kwake kwa ajili ya kumkamata alikimbia, ingawa hakufika mbali baada ya kuona nyumba yake inabomolewa, walipomsogelea na kutaka kumkamata ili kumfikisha Kituo cha Polisi Sanya Juu, alikimbia tena na kukimbizwa na kukamatwa kijiji cha jirani," alidai.

Aliendelea kusimulia kuwa alipokamatwa, walimshambulia maeneo mbalimbali ikiwamo kichwani na kumkata miguu yote.

Alisema jitihada za kumwokoa zilifanyika na wakati anakimbizwa Hospitali ya Kibong'oto, alifariki dunia.

Kaka wa marehemu, Innocent Mrema ameiomba serikali kufanya uchunguzi wa kina kwa kuwa mdogo wake amefanya tukio hilo baada ya kukuta ng'ombe huyo amefungwa shambani kwake.

"Tunaomba serikali ichukue hatua, maana huyu jirani (mlalamikaji) alimfunga ng'ombe wake shambani kwa marehemu, kitendo ambacho kilimkasirisha ndugu yetu na kufikia kufanya tukio hilo.

"Marehemu (Mrema) ni mtu mzuri tu sijui ni kwa nini wananchi waliamua kujichukulia sheria mkononi, hii imetuumiza sana kama familia," Mrema alisema.



Mwendesha Pikipiki akiwa amepakia viroba vya Mkaa akienda kuuza katika Kijiji cha Msanga Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani hivi karibuni. **PICHA: JUAMANNE JUMA**

# Wataka muswada Sheria ya Ndoa uwasilishwe bungeni

**Na Elizabeth Zaya**

UMOJA wa Wanawake Wanaotetea Wanawake na Wasichana Tanzania (TAPO) umeliomba Bunge litekeleze jukumu lake la kikatiba la kuishauri serikali kupeleka muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Sheria hiyo inaruhusu mtoto chini ya umri wa miaka 18 kuolewa kwa ridhaa ya mzazi.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi mkoani Dar es Salaam, wadau hao walisema licha ya serikali kupewa mwaka mmoja na mahakama kuibadilisha sheria hiyo, mpaka sasa haijatekeleza.

Mwaka 2016, Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi alifungua kesi kupinga kifungu cha 13 na 17 vya sheria ya ndoa, vinavyoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14, kwa kibali cha mahakama na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi.

Julai 8, 2016, Mahakama Kuu ilitoa hukumu ikikubali vifungu hivyo vya sheria ya ndoa, vinapingana na Katiba ya nchi kwa kuweka umri tofauti wa kuoa na kuolewa kati ya mtoto wa kike na wa kiume.

Gyumi alisema hukumu ya mahakama iliitaka serikali kupitia kwa Mwanasheria Mkuu, kujipanga ili kurekebisha vifungu hivyo tata vya sheria ndani ya mwaka mmoja. "Ni miaka mingi sasa imeshapita tangu amri hiyo itoke, lakini hakuna jitihada zozote zilizofanyika katika kutekeleza uamuzi huu," alisema.

Mawi Zahor ambaye ni mshirika wa TAPO, alisema ni muda mwafaka sasa kwa wabunge kuchukua hatua na kuhakikisha serikali inaleta muswada huo wa marekebisho bungeni.

Mawi alisema ndoa za utotoni zina madhara makubwa kwa wasichana kwa sababu wengi hushindwa kutimiza ndoto zao na hivyo kuishia kupata maumivu ya unyanyasaji.

Alipongeza hatua iliyochukuliwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, kupitia tamko lake aliolitoa hivi karibuni bungeni kwamba wiki ijayo wanatarajia kukaa na kufanya marekebisho ya sheria hiyo.

"Kauli hii imeonyesha msimamo wa wizara kuhusu suala hili, wadau tumelichukulia kwa uzito mkubwa na tunasubiri utekelezaji wake kwa ajili ya maslahi ya watoto na wasichana wa Tanzania," alisema Mawi.

## Menejimenti yaridhishwa ujenzi nyumba za majaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MENEJIMENTI ya Mahakama Kuu ya Tanzania imeridhishwa na ujenzi wa nyumba za majaji wa Mahakama Kuu unaoendelea eneo la Iyumbu jijini Dodoma, sasa ukiwa umefika asilimia 70.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alibainisha hayo juzi wakati wa ziara fupi iliyojumuisha Menejimenti ya Watumishi wa Mahakama waliotembelea majengo hayo ili kuona ujenzi wa nyumba hizo unavyoendelea.

Prof. Ole Gabriel, alisema majengo hayo yanatarajiwa kukabidhiwa Desemba 31 mwaka huu ili yaanze kutumika kama walivyokubaliana na makandarasi wa mradi huo.

"Haya majengo yanatarajiwa kukamilika Desemba 31 mwaka huu na ninaamini makandarasi watatimiza makubaliano yaliyowekwa na serikali," alisema.

Prof. Ole Gabriel, alifafanua zaidi ya kuwa wanafanya hivyo kwa lengo la kutimiza ahadi ya serikali kwamba mahakama itahamia Dodoma kama zilivyofanya taasisi na wizara mbalimbali.

Kuhusu gharama za ujenzi wa nyumba hizo, kiongozi huyo alisema wanatarajiwa kutumia Sh. billioni 129.7 hadi kukamilika kwake.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutoa fedha za ujenzi wa majengo haya ya mahakama, tunaamini majaji watafanya kazi wakiwa katika mazingira rafiki yanayoendana na kazi zao," alisema.

Msanifu Majengo, Rose Nestori, aliwaomba wajumbe kutoka Mahakama ya Tanzania kutokuwa na wasiwasi wowote kwa sababu majengo hayo yatakamilika kwa wakati uliopangwa.

Rose alisema, wanaishukuru serikali kutokana na kutoa ushirikiano katika ujenzi huo ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri.

Mkurugenzi wa Rasimali Watu wa Mahakama ya Tanzania, Beatrice Patrick, alimpongeza Mtendaji Mkuu wa Mahakama kutokana na usimamizi mzuri wanaofanya katika ujenzi huo.

Alisema, wao kama wajumbe kutoka Mahakama ya Tanzania, wameridhishwa na ujenzi huo, hivyo wanaishukuru serikali kutokana na juhudi zake katika kuhakikisha mahakama hiyo inahamia Dodoma.

"Kwa kweli kabla hatujaona hatukutegemea kama tutakuta majengo kama haya. Ni hatua kubwa sana, hongereni makandarasi kwa kazi nzuri mnayoifanya," alipongeza.

Alitoa wito kwa makandarasi hao kutobweteka, badala yake waongeze bidii katika ujenzi wanaofanya ili waukamilishe kwa wakati.

# MAISHA

SEPTEMBA 18, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13

**Msimu wa suruali nyepesi**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Pamba chumba kwa viti vya zamani



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Ondoa madoa usoni mwako

Ukurasa 14

## WATOTO

MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | K | A | M | B | A |
| ■ | A | ■ | ■ | O | ■ |
| O | T | A | ■ | M | ■ |
| ■ | A | ■ | Z | O | A |
| ■ | Z | ■ | ■ | K | ■ |
| M | A | M | B | A | ■ |


## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI





## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UMO, PAA, KAMBI, JUMBA, BOMANI, JAMBIA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Musa alikuwa akizungumza na mama yake, katika maongezi yao alianza kumuuliza kuhusu asali.

**Musa:** Eti mama, kila mlamba asali huwa anarudia?

**Mama:** Ndio mwanangu, hiyo ni kutokana na utamu wa asali.

**Musa:** Kwa hiyo kila anayelamba asali lazima achonge mzinga?

**Mama:** hapana mwanangu, mzinga wanachonga wafugaji na sio walaji

**Musa:** Mbona mwalimu katuambia ukionja asali lazima urudie?

**Mama;** Huo ni msemo tu, akimaanisha kila mtu anayefanya jambo kwa ubaya lazima atarudia kama hataonywa.

**SWALI**

Ziwa Rukwa linapatikana mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Huwezi kudharau na kusahau wazazi wako ukabaki salama

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vituko vya Maisha Ndivyo Yalivyo katika jamii yetu kila iitwapo leo. Bila shaka kwa wale waliofuatilia kisa cha kijana Selestine, walijionea ndoto yake ya kuwa tajiri kupitia waganga wa jadi ilivyoyeyuka na sasa ni miaka 11 hana chochote cha kujivunia.***

Leo msomaji wangu nikupitishe kuhusu uhusiano wa vijana na wazazi wao. Yamkini kijana Selestine angewashirikisha wazazi wake kuhusu ndoto yake katika maisha, yote yaliyomkuta yasingekuwapo.

Angeweza kuendelea na kazi yake ya kuchoma mkaa pengine leo angekuwa na uwezo mkubwa kiuchumi kwa mtaji uliotokana na biashara hiyo.

Wazazi ni walezi wakuu wa familia. Hawa ni watangulizi na yako mengi wamepitia. Hivyo, kama kijana anayeanza maisha yakupasa kumshirikisha mzazi,au wazazi au walezi ili wakushauri jinsi ya kuenenda kimaisha.

Na pale unaposhauriwa, sikiliza kwa makini, usiwabeze na kuwadharau, usiwaache pembeni na kwenda kutaka ushauri kwa watu ambao unaona wao ni maarufu kwako. Hatukatai kupata ushauri kwa watu wengine. Ni jambo jema sana.

> **"Waheshimu baba yako, na mama yako, kama BWANA, Mungu wako alivyokuamuru, siku zako zipate kuzidi, nawe upate kufanikiwa katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.**

Pamoja na hayo, ujue wako washauri wazuri na pia wabaya. Angalia Selestine aliwaendea marafiki kwa ushauri wakamwelekeza kwa waganga na ndoto yake ikaishia hapo. Wazazi wako ni chimbuko lako na nafasi yao iko pale pale. Haitakiwi kuchukuliwa na mtu mwingine.

Mara nyingi sana vijana wengi, mfano kipindi kile wanapofikia kuanza kazi au kuoa/kuolewa, wanakumbana na changamoto kubwa sana. Kijana anapofikia kuoa anaona nimwambie baba ya nini? Anakuja kumwambia mambo yote wameshamaliza.

Kutoka vyuoni wameshazunguka ndipo anakuja na kumwambia baba nataka kuoa binti huyu. Kumbe ni ndugu wa familia hakupasa kumuoa. Akiambiwa siyo chaguo sahihi anatishia kujiua (kisa hiki nitakieleza makala zijazo).

Jamani, sikiliza ushauri wa wazazi wako. Hata Mungu anasema katika moja ya andiko lake kwamba: "Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe". Taka ushauri kwa Mungu, taka ushauri kwa wazazi ambao Mungu amekupitishia kwao (wamekuzaa).

Wazazi wapo, hupaswi kutegemea akili zako, waambie unachopitia wakushauri ili kukuepusha na mabaya! Yaani kijana akimbilie kujiua kwa sababu tu ya kutotaka ushauri wa wazazi? Fanya uchunguzi wa kile wanachokushauri. Je, ni sahihi? Je, wao ndio sahihi au wewe ndiye sahihi?

Fanya upembuzi yakinifu ujiridhishe! Kwa hiyo hivi ni vitu vya kuangalia na vya msingi sana katika maisha yako wewe kijana kuona kwamba ni vizuri kusikiliza ushauri wa wazazi. Siku zote mzazi analo neno kutoka kwake kwenda kwa mtoto wake.

Hakuna mzazi ambaye anawaza mabaya kwa mtoto wake. Kwa hiyo wanapokushauri usione kwamba wanawaza mabaya kwako na eti hawakutakii mema. Ushauri wao ni kukutakia mema. Kama Mungu anavyosema kwenye neno lake, "ninayowawazia ninyi ni mema na siyo mabaya".

Wasikilize wazazi wako, huenda ipo siku utakumbuka yale maneno waliyokushauri ukasema; baba aliongea jambo hili, na mama aliongea hili.

Hivyo, kutokana yale wanayokushauri wazazi, basi baraka za Mungu zitaendelea kutembea na wewe katika maisha yako! Ndio maana Mungu akaweka mapema kwenye amri zake mbele ya wanadamu. Na kwa vijana akaweka amri kwamba;

"Waheshimu baba yako, na mama yako, kama BWANA, Mungu wako alivyokuamuru, siku zako zipate kuzidi, nawe upate kufanikiwa katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako".

Amri hii imeambatana na ahadi ya Mungu kwamba kwa kuheshimu wazazi, siku za kuishi zitazidi na pia, utafanikiwa kimaisha. Yamkini watu wengi leo hawafanikiwi kwa kuipuuzia amri hii. Waliwadharau au kutoheshimu wazazi wao matokeo yake wamekwama kimaisha.

Wapo waliowatukana wazazi wao, wengine wamewaua kabisa pengine kwa kugombania mali/urithi au kwa kulaghaiwa na washirikina eti wawafanyie hili na lile wazazi wao ili wapate utajiri. Hata pale walipotimiza masharti hayo maovu wakajikuta wanaishia pabaya.

***Mpenzi msomaji, bila shaka umeweza kujifunza kitu kwenye ujumbe huu kwa vijana wetu. Dharau na kutoheshimu wazazi ni janga kubwa kwa vijana. Je, una kisa au maoni? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Kuzuia madereva mtandao kufanya kazi ni kuumiza nchi

NIMEPATA bahati ya kutembea duniani na kila nilikokwenda baada ya kutua, nilitumia usafiri wa mtandaoni kwa maana ya teksi au gari la hoteli ninayofikia.

Katika viwanja vya ndege vya zaidi ya nchi 20, nilizotembelea zikiwamo nyingi za Afrika, sijaona madereva mtandaoni wakikatazwa kuingia uwanjani kubeba abiria. Nilikwenda mbali zaidi nikauliza kama madereva hao wanakatazwa pia kuingia kwenye kituo kikuu cha mabasi kwa ajili ya kupakia abiria.

Kwenye baadhi ya nchi kama Afrika Kusini katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa OR Tambo, Johannesburg, wanakutangazia kabisa aina zote za usafiri ikiwamo teksi mtandao za kampuni fulani na fulani zinapatikana eneo fulani, hivyo ni wajibu wako kuchagua aina ya usafiri unapowasili.

Kwa nchini kwetu, ni tofauti kabisa kwamba madereva wa magari ya mtandaoni wanapoingia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), au Kituo cha Mabasi ya Magufuli, wanatozwa faini na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege au uongozi wa stendi.

Kama haitoshi kuna tangazo limebandikwa kuwa hawaruhusiwi kuegesha gari kwenye viwanja hivyo lakini wanapoingia na kutoka wanaingiza mapato kwa uwanja kwa kuwa kila gari inalipa Sh.2,000 kwa saa katika uwanja huo.

Teksi mtandao zimetoa ajira kwa vijana wengi na zinalipa mapato mengi kwa serikali lakini kila siku vikwazo vinaongezeka ili kuwalinda madereva teksi ambao hawapo mtandaoni.

Sielewi ni kwa nini maofisa wa serikali wa eneo hilo wanazuia teksi mtandao wakati ndio zingeingiza mapato mengi sana kwa kuwa abiria wanaziita,pia madereva wa taxi za kawaida wangejiunga huko na ingeongeza mzunguko.

Lakini, abiria unalazimishwa kuchukua teksi unazozikuta nje ambazo bei zake ni kubwa na imefikia mahali wanapokushawishi uwakodi wanakwambia nitakutoza bei ya Uber au Bolt (magari ya teksi mtandao), maana yake wanajua kila mtu anafuata urahisi.

Kwa viwanja vya ndege husussan Dar es Salaam hata kama wewe ni mmiliki wa gari la teksi mtandaoni huwezi kumwita dereva akubebe kwa sababu atakamatwa na kutozwa faini ili asiingie humo ndani na wameweka tangazo kubwa la kukataza magari hayo.

Kwangu nahesabu haya ni manyanyaso kwa abiria na madereva ambao wengi ni vijana wanajitafutia riziki. Wananulipa kodi ya mapato, wananunua mafuta, wanalipa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), jiji na manispaa zote. Hizi ni kodi ambazo lazima zilipwe ndipo gari liingie barabarani.

Badala ya kusaidia biashara hii kustawi sasa inakufa sijui ni kwa maslahi ya nani? Kwa sasa kampuni maarufu za Uber na Bolt zimeondoa biashara kutokana na kushindwa kuelewana na serikali, wanaoumia ni vijana wengi ambao walitegemea biashara hiyo kuendesha maisha yao.

Tatizo la ajira ni kubwa sana nchini kwa sasa. Hali ya maisha inazidi kuwa ngumu na watu wanapojikwamua kwa shughuli halali bado wanawekewa vikwazo na haohao ambao wanatoa vibali kazi hiyo kufanyika.

Kama nchi zenye uchumi mkubwa zinaruhusu taxi hizi kufanya kazi kokote kwanini kwetu zinazuiwa kwanini itumike nguvu kubwa kuwalinda madereva teksi wa kawaida kwa kuwa wanachama chao bila kuangalia soko huria lililopo?

Hivi karibuni uliibuka mgogoro mkubwa baada ya serikali kupiga marufuku magari kupakia na kushusha kwenye vituo binafsi, wakitakiwa kushusha abiria wote kituo cha Magufuli tu. Sababu kubwa ni kufanya biashara ya teksi na bajaji iendelee kuwapo kwa sababu wamelipa mapato.

Pia, kwenye kituo hicho teksi mtandaoni haziruhusiwi kupakia wala kushusha na kuna watu maalum wa kuwakamata,hii sio sawa kabisa ni kulinda kundi la wachache kwa faida ya wachache huku wengi wakiumia.

Kila siku nchi inazungumzia tatizo la ajira. Hiki kinachoonyesha kuajiri wengi na kurahisisha usafiri kwa umma kinawekewa vikwazo vingi,ni ngumu sana kupunguza ukali wa maisha kwa muundo huu.

Tumeshaingia kwenye biashara huria lazima baadhi ya viongozi waondoe urasimu na ubinafsi. Kama hawa madereva wa kawaida wanaonekana muhimu sana washawishiwe kujiunga kwenye teksi mtandao kuliko myanyanyaso tunayoyaona sasa.

Kwa nini wasafiri wa anga wateseke wasipewe uhuru wa kuchagua aina ya usafiri wa kutumia? Kwa nini madereva mtandao wanaolipa kodi kama wengine wanyanyasike nchini mwao?

Mathalani, hivi karibuni nilishuhudia mgogoro wa madereva na askari JNIA, aliwakamta wanne na kuwasomea sheria za uwanjani humo kwamba hawaruhusiwi kabisa kuegesha gari bali washushe watoke nje wakiitwa warudi tena.

Yote haya ya nini? Kwa nchi ambayo inatambua biashara ya ushindani na umuhimu wa watu wake kulipa kodi,kunapoongezeka vikwazo kila kukicha ni kuwafanya watu watafute mbinu chafu za kujipatia kipato.

Mathalani, tuna vijana wengi kwenye eneo hili,vikwazo vinapokuwa vingi maana yake wataingia kwenye shughuli nyingine mbaya ili kujipatia kipato, hivyo ni muhimu sana viongozi wanaofanya maamuzi wasiyaangalie maisha kwa jicho lao kwa sababu wana kipato bali kwa jicho la mwananchi wa kawaida kabisa kwa kuwa wanaishi kwa kodi za watu hao hao.

Haifai kupunguza walipakodi bali kuboresha mazingira ya kuongeza mawanda ya kodi, mazingira bora ya watu kupata fedha na kulipa kodi. Ungewekwa utaratibu wa madereva hawa kufanya kazi bila usumbufu kwa manufaa yao na nchi kwa ujumla.

***Mungu ibariki nchi yangu.***

# HARUSI





Unaweza kutengeneza nguo za harusi kwa kutumia vitambaa vyenye asili ya Kiafrika kama inavyoonekana pichani





# MITINDO







## Msimu wa suruali nyepesi

INGAWA suruali nyepesi inaweza kuvaliwa katika nyakati zote, lakini wakati wa kiangazi inafaa zaidi kutokana na kuwa na hali ya joto.

Katika kipindi hiki ambacho joto la kiangazi limeanza ni wakati mzuri wa kuvaa suruali ya aina hii pamoja na nguo zingine ambazo sio nzito na kukusababishia usumbufu.

Kutokana na umuhimu wa vazi hili, haya ni baadhi ya maoni bora ya kuchanganya mavazi yako kwa miezi michache ijayo.


"Suruali nyepesi hufanya kazi nzuri na iwe ya rangi inayopitisha mwanga, unganisha na fulana yenye mistari ya baharia au shati la kupendeza la jeupe ili kukupa mwonekano mzuri wakati wa joto" anasema Chuma.

Charles anasema "Suruali ya mavazi ya rangi nyepesi ni nzuri kwa blazi ambayo unaweza kuwa nayo kwenye kabati lako. Ikiwa unachagua suruali nyeupe, una chaguzi nyingi kwa suala la rangi ya koti ya kahawia, bluu bahari na udhurungi.Unachagua kulingana na hafla na mahali unapokwenda,"

Christopher anasema "Njia rahisi sana ya kupata unadhifu msimu huu wa joto ni kuvaa suruali ya kijivu na kuongeza nguo nyeupe hapo juu. Unaamua ikiwa ni shatii la polo au shati la mikono mifupi."

UREMBO







# Ondoa madoa usoni

NGOZI inatakiwa kujitengeneza yenyewe na si kuitengeneza kwa vipodozi kama wengi wanavyodhani.

Ulaji wa matunda na mboga za majani kwa wingi na kunywa maji ni njia nzuri kama unataka kuwa na ngozi nzuri isiyo na madoa wala kavu.

Wengi wanaacha kula mbogamboga na matunda kwa wingi hata kutokunywa maji ya kutosha na badala yake wamekuwa wakitegemea kuwa na ngozi nzuri jambo ambalo ni gumu.

Mara kadhaa tumeshuhudia watu wanaopaka krimu kali na kuharibika muonekano na kuwa kama wameungua usoni na mwili ukionekana na makovu.

Kuna watu wamekuwa na ngozi za asili na hata unapowauliza baadhi yao hawajawahi kupaka krimu lakini wana ngozi nzuri zinazovutia.

Unaweza kutibu ngozi yenye madoa usoni pia mashavuni kwa kujitibu na juisi ya limao.

**Namna ya kufanya**

Chukua limao lioshe na kisha likamue na kuchuja mbegu zake. Weka juisi hiyo kwenye kikombe na kisha tafuta kitambaa laini kichovye kwenye juisi ya limao na dondoshea kwenye sehemu zenye tatizo.

Kaa kama dakika tano kisha osha uso kwa maji safi. Pia unaweza kuchanganya na asali mbichi na maji ya limao husaidia pia kuondoa madoa usoni.

Limao lina sifa kubwa ya kuzuia harufu pia unaweza kulitumia katika kuondoa harufu kali ya jasho mwilini na husaidia kuondoa weusi kwenye kwapa, chini ya macho na mapajani.

Chukua kipande cha limao weka sukari kidogo, sugua.Unatakiwa kutumia kwenye kwapa ambalo ni safi, vizuri kutumia njia hii kabla na baada ya kuoga.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mtindi unakata uzito

KUPITIA kona yetu ya mapishi wiki iliyopita tulieleza maajabu ya mayai katika kupunguza mwili wenye uzito mkubwa.

Leo tunaendelea kukueleza baadhi ya vyakula vitakavyokusaidia kupunguza mwili na kuwa na afya njema.

**MTINDI**

Huu ni mfano wa chakula kilichothibitishwa kisayansi kusaidia katika kupunguza uzito kama mayai.

Hii ni kwa sababu mtindi una kiasi kikubwa cha Protini.

Tafiti nyingi za kisayansi zimeonyesha kuwa watu wanaokunywa mtindi asubuhi wameonekana kupunguza uzito haraka zaidi ya wale wasiokunywa.

**Jinsi ya kula mtindi kama kifungua kinywa**

Unaweza kutumia mtindi wenyewe au ukachanganya na vitu vingine ili kubadilisha ladha au kuongeza virutubisho zaidi.

Kwa mfano ili kuongeza protini zaidi kwenye chakula hiki unaweza kuchanganya na karanga au mbegu kama almonds na chia seeds.

Unaweza changanya na kipande kidogo cha tunda kama berries au kipande cha ndizi kwa ajili ya kuongeza utamu kwa mbali.



Robo lita tu ya maziwa haya wakati wa asubuhi hukufanya ujisikie umeshiba bila kuhitaji kitu zaidi.

Lakini kama bado utaona kama ni kidogo hakikisha aidha unaongeza mtindi kidogo au unaongeza karanga, almonds, chiaseeds ili kuongeza protini zikushibishe zaidi.

Hapa tunaongelea mchemsho aidha wa nyama, samaki, njegere au wa mboga mboga bila chapati, ndizi na vyakula vingine vya wanga.

Kama kawaida uzuri wake ni kwamba ni chakula kinachojengwa hasa na protini.

Usisahau kutumia angalau mafuta kidogo kwenye mchemsho wa mboga mboga badala ya kuchemsha chukuchuku.

Mafuta yana kazi yake katika mwili wa binadamu, haitadhuru hata kidogo kupikia angalau kijiko kidogo kimoja cha mafuta.

**SMOOTHIE**

Huu ni mchanganyiko wa maziwa na tunda au mboga mboga unaovurugwa kwenye blenda ili kutengeneza kinywaji mfano wa milk shake.

Jinsi ya kutengeneza smoothie

Changanya matunda yasiyo na sukari sana kama strawberries, zabibu, mafyulis (Peaches), parachichi, kwenye maziwa kisha saga kwenye blenda.

Ili kuongeza virutubisho zaidi hasa protini unaweza kuongeza kijiko cha siagi ya karanga au karanga.

Unaweza pia kutumia kipande kidogo cha tunda lenye sukari kama hauna uzito mkubwa sana au kijiko cha asali kwa ajili ya kuongeza utamu wake.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

## Pamba chumba kwa viti vya zamani



MAPAMBO katika nyumba ni jambo la kuzingatiwa kwa lengo la kuiweka katika mandhari inayovutia.

Moja ya mapambo ambayo wengi hawafahamu lakini yanaleta taswira nzuri ya nyumba ni viti vya zamani.

Viti vya zamani huleta matokeo mazuri ndani ya nyumba na kama ukipangilia vyema, kila mtu anapoingia na kutoka lazima ataisifu nyumba yako.

Hizi ni baadhi ya dondoo ambazo zifahamu jinsi ya kupamba viti vya zamani katika chumba cha chakula.

**1:** Weka viti na meza kulingana na ukubwa wa chumba, kama kidogo inafaa kuwa na viti vitano na meza moja.

**2:** Ukiweka katika mtindo wa duara itapendeza zaidi kwani ina mtazamo mzuri.

**3:** Kama viti vya samani sana, unaweza kuvisugua na kupaka rangi inayoonyesha uasili wake.

**4:** Hakikisha viti vimetengenezwa kwa mbao, ingawa kama una viti vya chuma vinafaa pia.





# Weka mifumo bora ya kuzuia majanga moto kwenye nyumba

USALAMA wa nyumba ndiyo jambo la msingi kuliko vyote katika ustawi wake.

Mbali na vitu vingine ambavyo ni muhimu katika nyumba kuanzia maandalizi, wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi ni pamoja na kuweka mfumo mzuri wa kuepusha majanga ya moto.

Msanifu Majengo, Eliud Jumanne, anasema ziko njia mbalimbali za kutumia kukabiliana na majanga ya moto kwenye nyumba ikiwamo kutumia mfumo bora wa umeme.

Njia ya pili, anasema ni kutumia vizuri soketi na swichi ya umeme pamoja na kuepuka kutumia vifaa vya umeme duni vikiwamo redio, pasi, jokofu, televisheni na jiko.

"Kutokana na ujenzi duni, si jambo la kustaajabisha kukuta nyumba moja ina soketi moja au mbili. Hili husababisha watu kujaza kila kifaa kwenye soketi hiyo moja, na kusababisha soketi hiyo izidiwe na kuwaka moto," alisema.



Ya tatu, anasema ni kutumia vema jiko lililoko ndani ya nyumba.

"Jiko lililoko ndani ya nyumba unatakiwa kuchukua tahadhari zaidi. Haijalishi ni jiko la umeme, gesi au mafuta. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ili kuepuka majanga ya moto. Lisafishe, usiliache likiwa na mafuta au kuacha karatasi karibu nalo," anabainisha.

Njia ya nne, kwa mujibu wa mtaalamu huyo, ni kuepuka kuacha moto ukiwaka karibu na nyumba.

Anashauri pia kutumia moto ulio wazi kwa uangalifu na kwamba wakati mwingine watu huwasha vibatari, mishumaa au hata sigara ndani ya nyumba kwamba ni vyema kuandaa miundombinu na vitu vya kukabiliana na moto.

"Ni vyema kuchukua tahadhari kabla ya janga kutokea. Ni muhimu ukahakikisha nyumba yako ina miundombinu ya kukabili moto pamoja na vifaa vya kuzimia moto. Weka vifaa vya kuhisi moto au moshi.

"Hakikisha watu wanaweza kujiokoa kwa kupitia madirishani au kwenye milango ikiwa moto utatokea. Yaani jenga madirisha na milango inayoruhusu watu kujiokoa. Weka vifaa vya kuzimia moto kama vile mpira wa maji wa kuzimia moto pamoja na mitungi ya hewa," anasisitiza.


Anashauri usitumie vitu vinavyoshika moto haraka ikiwamo mafuta ya gari, rangi, gesi na pamba.

"Hakikisha unachunguza kila bidhaa unayotaka kuiweka kwenye nyumba yako ili kubaini kama inashika moto haraka ili ihifadhiwe kwa tahadhari kubwa."

Lingine analoshauri ni kuchukua tahadhari umeme unapokatika kwa kuzima vifaa vya umeme.

"Tumia vifaa vya kutawala kiwango cha umeme. Hivi huhakikisha umeme unaoingia kwenye vifaa vyako ni wa kiwango kinachotakiwa na huwa na mfumo unaojulikana kama "delay" ambao hauruhusu umeme kuingia kwenye vifaa moja kwa moja mara unaporudi."

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
!
'PANYARODI'
SISI
KWA HIYO BOSI UMESUSA NA KUNINUNIA KWA SABABU NIMEOLEWA AU SIO?
WEWE MWENYEWE UNADHANI SIFA? SEKRETARI UNAOLEWA KINAGAUBAGA!
HAKUNA PANYARODI PANYA YOTE NI SAWA TU, KAMA TAFUGA PAKA HAPANA ONA PANYA NARANDARANDA DANI YA JUMBANI YAKO
USHAYAVULIA NGUO JIANDAE KUYAOGA, UTAJUA KAMA UFUGE PAKA SHUME AU PAKA MAPEPE
TANDALE
MKABAJI KAKABWA
KWA TAARIFA YENU TUNAWAJUA MPAKA KWA WAZAZI WENU KAZI MNAYOOOO! HATUKUBALIII..
KWELI TUNA-TETA KIDIJITALI BILA KELELE KABISA
KIKAO CHA SIRI PANYARODI
KWA HIYO WEWE MPAKA LEO JIBU LA KUWA NA MKE BADO NI KIZUNGUMKUTI?
BABA KAMA KUSOMA UJUI HATA PICHA HUONI?
DUME ZIMA JUZI UMESIKIA 'MAPANGASHAA' WAPO MTAA WA PILI UKAANZA KUNYWA WIMA HUKU VIATU UMEVIWEKA KWAPANI!
KAMA UJUI HIYO INAITWA 'SELFU DIFENSI' MTAJI MBIO
GROSARI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
ATAYUMBAYUMBA LAKINI MLEVI HAPOTEI KWAKE

HABARI KIMATAIFA

# Putin adai hatishiki na mashambulizi mapya

**MOSCOW, Russia**

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amesema mashambulio yaliyofanyika hivi karibuni ya kukabiliana nchini Ukraine, hayatabadili mipango ya nchi hiyo.

Katika kauli yake ya kwanza kwa umma kuhusu vita hiyo, Putin alisema hana haraka na mashambulizi hayo na kwamba mapigano katika jimbo la Donbas yanaendelea.

Katika mashambulio ya haraka yaliyofanywa dhidi ya vikosi vya Russia, wanajeshi wa Ukraine waliweza kuteka eneo la kilomita za mraba 8,000, sawa na maili 3,000 za mraba katika kipindi cha siku sita katika jimbo la kaskazini-magharabi la Kharkiv.

Hata hivyo, Putin alisema kuwa Russia hadi sasa haijapeleka vikosi vyake kamili.

"Mashambulizi yetu katika Donbas hayakomi. Yanasonga mbele, sio kwa kasi sana lakini wanaendelea taratibu kuyateka maeneo zaidi na zaidi ," alisema baada ya mkutano katika Uzbekistan.

Mji wa viwanda wa jimbo la Donbas uliopo mashariki mwa Ukraine unalengwa katika uvamizi wa Russia, ambako Putin anadai ni muhimu kuuteka ili kunusuru wazungumzaji wa Kirusi na mauaji ya kimbari.

Sehemu za Donbas zilitwaliwa na wapiganaji wanaotaka kujitenga wanaoungwa mkono na Russia tangu mwaka 2014.

Jimbo la Kharkiv, ambako hivi karibuni Ukraine ilifanya mashambulio ya kukabiliana na uvamizi, sio sehemu ya Donbas.

Katika kauli ya siku ya Ijumaa, Putin alitishia kujibu vikali iwapo mashambulizi ya Ukraine yataendelea.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, amelituhumu jeshi la Russia kuwa la watesaji wakati maofisa wa nchi hiyo wakifukuwa miili ya watu kutoka makaburi ya halaiki yaliyo katika maeneo yaliyokaliwa Russia.

Miili ipatayo 400 imekwishapatikana katika eneo hilo hadi sasa.

Zelenskiy aliliambia shirika la habari la Reuters kuwa kuna ushahidi wa mateso na uhalifu wa kivita katika makaburi hayo ya pamoja katika mji wa Izium.

Rais huyo amelinganisha madhambi yanayodaiwa kufanywa na Russia katika mji huo na yale ya mjini Bucha, na kwa mara nyingine ametaka iundwe mahakama ya kimataifa kuchunguza uhalifu wa kivita nchini Ukraine. Gavana wa eneo hilo, Oleg Synegubov alisema asilimia 99 ya miili iliyofukuliwa inaonyesha alama za mateso.

**BBC**



Jeneza la Malkia Elizabeth II likiwa limewekwa ndani ya jengo la bunge la Uingereza la Westminster kwa ajili ya kuagwa na wananchi. **PICHA: AP**

# Viongozi wawasili Uingereza kumzika Malkia Elizabeth II

**LONDON, Uingereza**

VIONGOZI mbalimbali wa ulimwengu wameanza kukusanyika mjini London nchini Uingereza kuanzia jana kwa ajili ya kuhudhuria mazishi ya Malkia Elizabeth II.

Wana mfalme William na Harry waliongoza wajukuu wote wa Malkia kwenye shughuli ya kutoa heshima zao za mwisho kwenye jeneza lake.

Siku ya Ijumaa Mfalme wa Uingereza Charles wa tatu na ndugu zake walisimama karibu na jeneza la mama yao marehemu Malkia Elizabeth wa pili kutoa heshima zao huku maelfu ya waombolezaji wakiwa kwenye foleni ndefu wakisubiri kutoa heshima zao za mwisho kwa kiongozi wao.

Walielezwa kwamba huenda wangelisubiri kwenye foleni hiyo kwa saa 24 kabla ya kupata fursa ya kumuaga Malkia Elizabeth wa pili.

Mistari mirefu ilionekana kando ya Mto Thames tangu siku ya Jumatano wakati jeneza la malkia Elizabeth lilipoletwa kwenye jumba la bunge la Uingereza, Westminster.

Mfalme Charles wa tatu, Princess Anne, Prince Andrew na prince Edward, wakiwa wamevalia sare za kijeshi, walisimama kimya na kuinamisha vichwa vyao kwa dakika 15 katika Ukumbi wa kihistoria wa Westminster ambako jeneza la marehemu malkia wa Uingereza limewekwa hapo tangu siku ya Jumatano kwa ajili ya kuagwa kabla ya kuzikwa kesho.

Kifo cha malkia huyo wa Uingereza kilitokea mnamo Septemba 8 akiwa na umri wa miaka 96, baada ya kutawala kwa miaka 70 kwenye kiti cha enzi.

Mrithi wa malkia, Mfalme Charles III, alikutana jana mawaziri wakuu wa mataifa ya Jumuiya ya Madola ambayo ni makoloni 14 ya zamani ya Uingereza.

Australia, New Zealand na Canada, zimemtangaza rasmi kuwa Mfalme Charles wa tatu kuwa ni mtawala wao mpya.

Wananchi wa nchi hiyo una siku moja hafi kesho asubuhi kuaga mwili wa Malkia Elizabeth kabla ya kufanyika mazishi ya kwanza ya kiserikali nchini humo kwa karibu miongo sita

**DW**

## Museveni aapa kuendelea bomba la mafuta

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, ameapa kuendelea na mradi mkubwa wa bomba la mafuta la Afrika mashariki, akipuuza azimio la wabunge wa Ulaya lililotaka mradi huo ucheleweshwe kutokana na lilichokiita 'ukiukwaji wa haki za binadamu. Kampuni ya Total Energies ya Ufaransa na shirika la Taifa la Mafuta la China zilitia saini makubaliano ya dola bilioni 10 mapema mwaka huu ili kuendeleza visima vya mafuta ya Uganda na kusafirisha mafuta hayo ghafi kupitia bomba la urefu wa kilomita 1,445 hadi bandari ya Tanga nchini Tanzania kwenye bahari ya Hindi.

Mradi huo umekabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa wanaharakati wa haki za binadamu na makundi ya mazingira ambayo yanasema unatishia maisha ya makumi kwa maelfu ya watu na mifumo dhaifu ya ikolojia katika eneo hilo.

**DW**

## Wakuu wa nchi 150 kukutana Newyork

**NEWYORK, Marekani**

VIONGOZI wa nchi 150 wanatarajiwa kuwasili mjini New York kushiriki katika mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, wa kwanza wa ana kwa ana tangu kulipuka kwa janga la corona.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, ameruhusiwa kulihutubia baraza hilo kwa njia ya video, kutokana na vita vya uvamizi wa Russia vinavyoendelea katika nchi yake. Akizungumza kabla ya mkutano huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres alisema dunia inashuhudia mgawanyiko mbaya zaidi kuwahi kuonekana tangu kumalizika kwa enzi ya vita baridi.

Ingawa kura iliyopigwa katika baraza hilo imempa ruhusa rais Zelenskiy kutohudhuria mkutano huo, nchi saba, zikiwemo Russia na China zilipinga, zikisema haki hiyo inapaswa kuwaendea viongozi wote.

Rais Vladimir Putin wa Russia na Xi Jinping wa China pia hawana mpango wa kwenda mjini New York

**DW**

## MAKALA



Na Magabilo Masambu

# NDOTO YAKO NJEMA NI KINGA YA MAOVU

KUNA mambo mengi sana ya ovyo tunayafanya katika maisha kwa sababu hatuna ndoto ya kutimiza. Inawezekana hatujui hasa ndoto maana yake ni nini. Wengi tunadhani ndoto ni zile tunazoota tukiwa usingizini yaani unaota unafukuzwa na majambazi au unaota umeokota pesa kisha unajifariji kwamba iko siku utatimiza ndoto yako ya kuwa tajiri kwa staili hiyo.

Wako wanaodai kwamba ndoto ni sehemu ya mawazo yetu ya kila siku kwamba mambo mengi tunayoyaota huwa ni sehemu ya shughuli zetu za kila siku. Kwa kiasi fulani nalikubali maana nakumbuka nilipokuwa mdogo nikiwa kijijini, nilikuwa nachunga ng'ombe, usiku nilikuwa nikisikika mara kwa mara nikipiga miluzi kuashiria nawaelekeza ng'ombe kwenda mahali. Hizo ndizo ndoto tunazozijua wengi. Mtu mmoja amewahi kusema kwamba "Ndoto ni jambo linalokufanya usipate usingizi". Maana yake unalala lakini usingizi hauji kwa sababu unawaza namna ya kulitimiza. Prof. Tigiti Sengo, huwa anasema usingizi ni kwa ajili ya wapumbavu. Kwa mujibu wa Prof. Sengo, usingizi ni chanzo cha umaskini, hivyo huwezi kutimiza ndoto yako ikiwa utatumia muda mwingi kulala na kuota ndoto za kufukuzwa na panya.

Ndoto yako njema inakuwaje kinga ya maovu? Ukiwaza kutimiza mambo mazuri kwenye maisha, maana yake unajiepusha na mambo au tabia zinazoweza kusababisha usitimize ndoto yako. Ukiishi bila kuwa na ndoto njema, maana yake utashawishika kuingia kwenye tabia za ovyo kwa sababu huna unachotarajia maishani. Ni bora uwe na ndoto ya kuwa Rais kama aliyo nayo Raila Amolo Odinga wa Kenya, hata kama haitatimia lakini itakusaidia kuyakwepa mambo mengi machafu.

Vijana wengi tunajiingiza kwenye tabia za ovyo na hatarishi kwa sababu wengi wetu hatuna ndoto katika maisha yetu. Hatujawahi kufikiri kwamba utafika wakati ambao taifa na jamii kwa ujmla vitatutegemea maana wazee wa leo walikuwa vijana wa jana. Kuishi bila ndoto, hasa kwa sisi vijana, ni jambo hatari sana kwa maisha yetu binafsi lakini kwa maisha ya wengine pia.

Lakini si vijana tu, ndoto anatakiwa kuwa nayo kila mtu kwa sababu maisha hayaishi mpaka tunapoyapoteza na kuondoka duniani. Ukishakuwa na ndoto ya kutimiza kwenye maisha, kwanza utamheshimu na kumjali kila mtu kwa kuamini kwamba inawezekana mtu huyo uliye naye kesho anaweza kukuvusha mahali. Hii ndiyo kusema ukitaka kujua mtu anayeishiishi tu bila ndoto, huwa anaishi bila kujali watu maana anaamini hana cha kupoteza na mara zote anafikiria pale alipo ndiyo mwisho wake.

Nakubali kwamba tunatofautiana katika ndoto zenyewe na kutimiza ndoto haimaanishi mpaka ufike kiwango cha juu zaidi. Kuna mtu ndoto yake ni kuwa bwana shamba tu, yaani amekuwa anawaza tangu utoto wake kwamba siku moja awe na pindi anapokuwa, basi roho yake inajisikia murua kabisa. Inawezekana huwa akimwona bwana shamba kavalia buti zake zile, basi anapenda sana.

Ziko ndoto mbaya pia ndiyo maana nimesema ndoto njema. Kuna mtu ndoto yake ni kumuua Fulani. Yaani analala anaamka anasema lazima nitimize hili. Ni ndoto lakini ya kijinga kwa sababu inakupeleka kutenda uovu ambao utakugharimu. Ni kweli kwamba huwezi kuchagua ndoto ya kutimiza, bali ndoto lazima iwe sehemu ya kipawa chako. Huwezi kuwaza kutimiza ndoto ya kuwa mchezaji bora wa mpira duniani0, wakati wewe unapendelea muziki zaidi kuliko mpira.

Mbinu moja nzuri katika maisha, kama utagundua mapema kwamba unataka kuwa fulani huko mbele, basi huna budi kujenga uwezo katika eneo hilo hasa katika kujielimisha zaidi na kuwa mfuatiliaji wa jambo lenyewe. Unataka kuwa mwanasiasa bora, lazima uwe mfuatiliaji wa siasa. Kama wewe ni mhandisi wa majengo, bahati mbaya mazingira yalisababisha ukaenda huko, lakini kila wakati unawaza kuwa nahodha wa meli kubwa duniani, basi huna budi kubadili na uanze kuelekea kwenye kutimiza ndoto yako. using'ang'anie uhandisi wakati unaona kabisa hutaweza kuwa nahodha. Malengo jumlisha mipango itakupeleka kwenye kutimiza ndoto ambayo wengi huwa wanaita malengo. Unasikia mtu anasema nataka nitimize malengo yangu! Ukiwa na malengo hutakuwa mlevi wala 'panya road' maana wengi wanasingizia kwamba ni ugumu wa maisha. Unajiuliza kwa nini wote wenye ugumu wa maisha, waliyatatua kwa kuwa 'panya road'? Unakuta si kweli.

Ushauri wangu kwa vijana wenzangu na watu wote, kila mmoja atimize jambo jema katika maisha yake. Ikishakuwa hivyo tutapunguza uhalifu na maovu kwa sababu tunatarajia kuwa watu fulani kwenye jamii lakini zaidi tutasaidia ustawi wa watu wengine. Ukiwa mwalimu ukahisi hapo ulipo ndiyo mwisho utawaumiza wanafunzi wako. Ukiwa daktari, fikiria kuwa daktari wa kimataifa zaidi. Ukiwa polisi wa kawaida fikiria kuwa IGP siku moja na ukiwa askari wa jeshi ndoto yako siku moja uwe mkuu wa majeshi. Lakini ukiwa kijana wa nchi hii fikiria kuwa mtu muhimu leo na kesho katika taifa hili. Ukishawaza hivyo, hutakuwa kwenye makundi ya ovyo ovyo kwa kuwa utataka ndoto yako itimie.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO



Na Adam Fungamwango

# Mbaraka na 'Wajomba wamechacha', kisa cha bakora kutembezwa harusini

WAJOMBA wamechacha wamekuja juu harusini, wapi mahari mbona sisi hatujapata?" Huo ni utangulizi wa wimbo uitwao 'Wajomba Wamechacha' uliopigwa na Super Volcano iliyokuwa ikiongozwa na marehemu Mbaraka Mwinshehe.

Wimbo huu ulirekodiwa katikati ya miaka ya 1970, na kuwa moja ya wimbo maarufu sana nchini. Si tu kwamba ulitungwa na kupigwa na mwanamuziki maarufu, lakini hata maudhui ya wimbo huo yalikuwa ya kuwafurahisha wengi. Ulibeba dhana ya utamaduni wa Mtanzania na Mwafrika kwa ujumla, kuhusu mila na taratibu za kuoa.

Kuna makabila mila za Kiafrika mila za kuoa zinafanana au kutofautiana kidogo. Lakini ziko mila ambazo kutoka upande mmoja kwenda mwingine hazifanani kabisa. Lakini muoaji ndiye anatakiwa kufuata mila za mke mtarajiwa.

Kwenye mila kuna mambo mengi sana, unaweza kukuta barua au mahari wala si pesa nyingi, lakini kinachoangaliwa na kufuatiliwa kwa karibu ni utaratibu tu. Ukikiukwa unakuwa tafrani.

Katika maudhui ya wimbo huu, Mbaraka anazungumzia utaratibu wa kuoa kwenye mila la kabila la Kizaramo na Kiluguru, ambayo ana nasaba nayo. Hapa anazungumzia madhila yaliyotokana na mila kukiukwa. Inaweza kuonekana ni kitu kidogo sana lakini kimevunja sherehe nzima ya harusi.

Ni kwamba mahari imetolewa, lakini ndugu wengi wanalalamika hawajapata, haijulikani ni nani aliyepewa na kula.

Nimesema kwenye mila inawezekana ikawa pesa ndogo lakini wao wanachotaka utaratibu ufuate kila mtu aheshimike kwenye nafasi yake.

"Mwali hatoki mpaka sisi tukubali, muozeni lakini wajomba tuna radhi naye." Hao ni wajomba bado wanalalamika. Wamesimama mlangoni na kuapa kuwa mwali hatoki kwenda kwa mume mpaka wao wakubali na hata kama watamuoza kwa nguvu, basi wajomba hawana radhi naye.

Hapa inaonyesha nguvu ya wajomba kwenye makabila ya watu wa Pwani, hasa Wazaramo na Waluguru ambao kwao mjomba ndiye kila kitu. Mjomba wao ni kama mama na hii ni kwamba sababu yoyote anayeitwa mjomba ina maana amezaliwa na mama wa anayemwita hivyo. Inasemwa kuwa bila mjomba kukubali, hapo mke hupati hata kama baba mzazi akikubali.

"Babu na bibi 'swamula ndevu' hawajapata, wamewishasema bila hivyo hapakaliki." Kwenye harusi hii si wajomba tu, hata babu na bibi nao 'wamepigwa'. Hawajapata kitu chochote kwenye hiyo mahari. Wanataka pesa yao inayojulikana kama 'swamula ndevu.'

Hii ni pesa ya usumbufu kwa babu na hata bibi. Inaitwa hivyo kwa sababu wajukuu huwasumbua sana wazee kwa kuwavuta ndevu na vitu vingine vinavyofanana na hivyo. Hata mabibi nao wanapata taabu kwa wajukuu, hivyo kama ni binti akiolewa ni lazima kuna vipesa lazima wapate, ikiwa ni ishara ya kupoza usumbufu huo wakati akiwa mtoto.

"Kajaga lubuga' shangazi naye hajapata, bwana harusi ilibidi sasa kukimbia. 'wapi mwazoka' ndugu kwa ndugu kugombana, kisa mahari aliyokula hajulikani."

Kuna kitu kwa lugha ya kizaramo kinaitwa 'kajaga lubuga', yaani kanyanga uwanja. Shangazi mtu yeye anadai pesa yake ya kukanyagia uwanja. Na yeye pia kaja juu kiasi kwamba ikawa tafrani kwenye harusi hiyo kiasi sasa bwana harusi akaona isiwe shida, akatimua mbio.

Nadhani angeendelea kukaa angekutana na ndugu wengine wangedai kitu kinaitwa 'kakulongela nani kama hapa kuna mwali'. Hii pia ni pesa anayotozwa muoaji na ipo kwenye baadhi ya makabila ya Pwani, hasa Wazaramo na Waluguru, wakiwa na maana 'kakuambia nani kama hapa kuna mwali?'

Tafsiri ya hii ni kwamba kijana muoaji au yeyote yule aliyepeleka taarifa kuwa kuna mchumba wa kuoa pale, kile kitendo kwao ni kama ukosefu wa adabu, hivyo ni lazima kuwa na faini yake.

Baada ya bwana harusi kutimua mbio tai ikipepea, wakabaki ndugu kwa ndugu sasa kugombana, kila upande ukiwauliza wenzao 'nyinyi mnatokea wapi, mbona hatuwajui', au kama wanawajua, lakini hawahusiki. Lakini msingi wa yote hayo, mahari iliyotolewa haijulikani imekwenda wapi. Nani aliipokea na nani ameila? Mbona kila mtu hajapata?

Hii ni mikasa inayotokea sana kwenye jamii ambayo wanamuziki wa zamani walijitahidi sana kuiweka hadharani kwa sababu wao ni hadhira.

Ni mambo ambayo pamoja na kwamba yalitokea wakati huo, mpaka sasa bado yanatokea na yataendelea kutolea kizazi hadi kizazi. Ni kwa sababu watu wanazaliwa, wanakua, wanaoa na kuolewa na mila, taratibu na utamaduni bado vinaendelea.

Tatizo lililokuwapo tu ni kwamba, wanamuziki wa sasa hawaumizi vichwa kutafuta vitu vilivyojificha kwenye jamii hata kwenye masuala ya mapenzi. Wao ni mwendo wa 'nakupenda' tu. Nyimbo za mapenzi zimetamalaki.

Kwa sasa wanaonekana kwenda mbali zaidi. Sikiliza nyimbo nyingi za wasanii wa sasa. Wameshatoka kuimba mapenzi, wanaonekana sasa kuimba jinsi ya kufanya mapenzi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yoyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani. Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-19

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NA wale wengine niliowaua walikuwa ni akina nani? Na kwa nini alitaka wauwawe?"


"Nassor na Hassan wale ni mawakili ambao walikuwa na nyaraka zote za mali za baba yako. Walisubiri mtoto awe mkubwa na kufungua kesi. Sabri anafahamu kisa chote cha baba yako kuuawa na kutupwa kwenye korongo, alikuwa shahidi mzuri sana kwako, Hussein ni mjomba wa mama yako, kabla ya kujiua aliandika barua ya kwa nini anafanya hivyo, na akataka kama mtoto wake mdogo anayemuacha duniani akiwa mkubwa amkabidhi. Yaani alikuwa na barua yako akukabidhi ili ujue ukweli. Alimpigia simu akamwambia mjomba wake afike nyumbani mara moja na chini ya meza kuna barua ataikuta. Alifika na kukuta amejiua, lakini akaipata hiyo barua. Miaka ilivyozidi kwenda mzee Pokwa aligundua hilo, akawa anamuwinda kumuua ili kuzuia kitu chochote kisijulikane. Wewe pia ukahusika kufanya mauaji."

Prince alishusha pumzi kwa nguvu. Ni kama vile mtu aliyeutua mzigo uliokuwa unamuelemea kwa muda mrefu.

"Nashukuru mama kwa kunifungua macho. Binafsi kujua mzizi wangu ulipotokea ni kitu kikubwa kwenye maisha yangu. Ina maana ningekufa nisijue nimezaliwa na nani na mimi ni nani. Siwezi kusema ni akili yangu, au uwezo ila ni Mungu tu. Ni Mungu tu ndiye aliyesababisha yote haya, kwa sababu nakumbuka kuwa jana nilikuja nikuue. Ungekufa haya yote nisingeyajua. Pia, tumshukuru sana Hasnat, yeye ndiye aliyesababisha nisikuue na kupata ukweli huu. Mapenzi yangu kwake yamesababisha haya. Lakini naweza kusema kila kitu kilichotokea kimepangwa na Mungu." Akasema na kuanza tena kulia.

Hidaya, baada ya kumaliza kumpa historia nzima ambayo Prince alikuwa haijui, alinyanyuka kivivu na macho yake yakamuangalia binti yake.

"Mbembeleze mwenzio, mimi naenda kupakua chakula." Akaanza kuvuta hatua kadhaa kuelekea jikoni kwenye chakula ambacho awali kiliinjikwa na kupikwa na Hasnat. "Nyamaza Prince, kumbe yamekukuta mambo mazito hivi. Ulikuwa na haki ya kufanya ulichokuwa unafanya. Ulijua kuwa mama yako ameuawa kwa watu waliodhulumu mashamba ya wazazi wake, lakini kumbe si kweli. Aliyewaua ndiyo huyo anayekutuma uwauwe watu ambayo siyo, huku yeye mwenyewe akiwa anajua nini kinaendelea. Hi huzuni kubwa hata kwangu kujua kumbe baba na mama yako wote ni marehemu. Na muuaji ndiye anayekucheza shere. Anazidi kukudidimiza kwenye lindi la matatizo. Umelelewa ukiwa mpweke. Lakini angalia leo upo kwa mama yangu. Upo kwa mtu ambaye anawafahamu wazazi wako kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Basi usilie, hapa ni kama nyumbani kwako. Ni kama upo kwa mama yako tu. Na mimi pia nipo. Nipo kwa ajili yako. Nipo kwa ajili ya kukurejeshea furaha ambayo hukuwa nayo tangu mdogo."




**"Okay, ndiyo maana majina yenu yanafanana na baadhi ya askari wenzangu wakadhani kama namba hiyo ilikuwa ni yako, uligeuza majina tu kwenye kusajili."**

Maneno hayo yalimuingia Prince. Akashangaa maneno mazito kuongewa na msichana mdogo kama yule. Akajikuta akimshika mkono, akamvuta na kumkumbatia kwa nguvu.

Joto la kila mmoja, lilimuingia mwenzake na kutengeneza hisia kali kiasi kwamba walibaki wamekumbatiana mpaka Hidaya alipotoka akiwa na 'hotpot' ya chakula, sahani na vijiko.

Hakutegemea kuwakuta katika hali ile. Alisita, akasimama kidogo. Hakutaka wajisikie vibaya, akaanza kuelekea mezani kana kwamba hakuna kitu alichoona.

Walishtuka nao walipoona mama ametoka jikoni, wakaachiana na kutazamana kwa tabasamu pana, kila mmoja akionekana kuwa na hamu na mwenzake.

"Enhe mwanangu sasa nini kinaendelea?" Hidaya alitaka kujua msimamo wa Prince wakati kila mmoja chakula kikiteketea tumboni mwake.

"We acha tu mama, kichwa hapa kinaniuma. Ninachoshukuru ni kwamba kumbe nimefika nyumbani. Hapa ndipo nyumbani kwangu."

"Kwa baba yako hurudi tena?" Lilionekana ni swali la utani lililoulizwa na Hasnat kuelekea kwa Prince. Aliliuliza huku akikata na kutafuna kipande cha nyama.

"Hili niachieni mimi. Mimi nitaumaliza tu huu mchezo." Akajibu Prince akimungalia Hidaya kana kwamba ndiye aliyeuliza swali hilo. "Nakuomba mwanangu, kama utarudi huko kwa mzee Simon Pokwa, kuwa makini sana. Usifanye chochote kukuhatarishia maisha yako. Kuwa makini na wewe mwenyewe. Unajua mimi ni mtu wa mwisho kutumwa uniue, huwezi kujua baada ya hapo nini amepanga."

"Ni kweli mama nitakwenda nikiwa makini kuliko ilivyowahi kuwa mwanzo. Yule ni mzee mwerevu na mjanja sana inavyoonekana, inawezekana kabisa hata akahisi kuwa kuna kitu nimetambua, nikiwa makini sana."

******************************

"We mzee hufai kuishi hapa duniani. Hivi baba yangu alikukosea nini? Kwani kupenda kunalazimishwa?" "Wewe aliyekuambia huo upuuzi ni nani?"

"Hivi unadhani unaweza kuficha ukweli muda wote? Unaweza kuuficha kwa muda tu." Mzee Pokwa alicheka kwa dharau halafu akasema. "Kijana nadhani sasa umekua. Nilikulea ukiwa bado kifaranga, hivi ningekuwa mbaya au katili kama unavyodhani si ningekuminya tu wakati ule?"

"Ulikuwa ni mpango wako maalum ili mimi ndiyo nikufanyie kazi yako. Na ndicho kisa cha wewe kunifundisha kulenga shabaha. ukanifundisha kuua." Prince akajibu kwa hasira.

"Vizuri, umeshakutana na wajuzi wamekwambia eee. Sasa nakuhakikishia kwa sababu umeshaambiwa yote ya ukweli na ya uongo, humu ndani huwezi kutoka hai." Ilikuwa ni sauti ya upole ya mzee Pokwa, lakini ilikuwa na kutisha na ya msisitizo.

Prince baada ya kutoka kwa Hidaya, alionekana kubadilika kabisa. Alipofika kwa aliyedhani ni baba yake alionyesha kuwa amechukia sana.

Baba yake alimuuliza baadhi ya maswali, lakini mengine alijibu kwa ujeuri, mengine hakujibu kabisa. Akahisi kitu. Alipoanza kupasuka maneno aliyoambiwa na Hidaya, ndipo mzee Pokwa alipojua kuwa rasmi sasa yote aliyoyaficha miaka mingi iliyopita, yamejulikana.

"Unataka kuniua kama ulivyomuua baba na mama yangu?"

"Tena afadhali yao, wewe nitakuua, halafu nakufukia humu humu ndani kama paka aliyeiba mboga. Huna hadhi ya kuzikwa kama binadamu wengine."

"Haina shida, siogopi kufa. Kama baba na mama yangu wamekufa, sembuse mimi waliyenizaa niogope, ila nataka unithibitihie kuwa ni kweli umefanya hivyo?" "Kwa sababu umetaka mwenyewe na pia hata ufanyaje nini huwezi kutoka tena humu ukiwa hai, kila kitu ulichoelezwa ni kweli tupu." Pokwa alijitapa kwa dharau.

"Utalipa kwa ulichokifanya." Neno hilo lilisababisha kicheko kikali cha dharau kutoka kwa mzee Pokwa.

"Unajiamini sana kijana eee, ujanja wote na kazi hii nimekufundisha mimi, kwa hiyo niko mara 10 zaidi yako." Akamjibu.

Licha ya yote, bado Simon Pokwa aliendelea kushangaa ujasiri wa Prince, kwani pamoja na vitisho vyote, ambayo ni vya kweli, lakini hakuonekana kubabaika wala kuogopa.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# Starshine ampongeza Ommy Dimpoz

MSANII kinda wa Bongo Fleva, Starshine Tz, amempongeza Ommy Dimpoz kwa kuwa wazi kuwa hana ukaribu na baba yake mzazi.

Akizungumza na NIPASHE, Starshine anayetamba na wimbo, Ananivuruga, amesema Ommy Dimpoz amekuwa mfano kutokana na kuongea ukweli wake tofauti na wasanii wengine ambao wanaishi maisha feki.

Amesema, alichozungumza msanii huyo kuwa aliteleke-zwa ni funzo kwa wanaume wote wanaowatupa watoto wao.

"Nimependa Ommy Dimpoz, ambavyo ameamua kuwa muwazi wa kula mafanikio yake mwenyewe na wale aliohangaika nao na sio baba mbaye hakumlea utotoni, sisi wanaume tunapaswa kujifunza na kuwatunza watoto wetu ili watusaidie uzeeni," amesema Starshine.


# Vigogo wamzika babu wa msanii YJ

VIONGOZI mbalimbali wa serikali jana walijitokeza visiwani Zanzibar, kumzika babu wa msanii YJ ambaye ni Askofu Mstaafu wa kanisa la Anglican, John Ramadhani.

John Ramadhani, alifariki dunia mapema wiki hii katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Akizungumza na Nipashe jana, YJ amesema kifo cha babu yake ni pigo kwake kwani kupitia kwake amejifunza mengi.

"Hii ni heshima kwa familia yetu kuona viongozi kuja kumzika babu yangu hapa Zanzibar, imenifundisha kuishi na watu vizuri na kuwa mnyenyekevu ili Mungu azidi kukuinua," amesema YJ ambaye kwa sasa anatamba na wimbo wa Kizaizai akiwashirikisha Baba Levo na Billnas.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### TIELEMANS ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili kiungo wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans katika dirisha la Januari. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anakaribia kumaliza mkataba wake pale kwenye Uwanja wa King Power. ***(Fichajes via Leicester Mercury)***

#### LIVERPOOL, UNITED VITANI

LIVERPOOL na Manchester United zinanawania kumsajili kiungo wa Flamengo mwenye umri wa miaka 21, Joao Gomes katika dirisha la Januari. ***(Liverpool Echo)***

#### XEKA ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inataka kumsajili nyota mwenye umri wa miaka 27, Xeka kutoka Lille ambako kwa sasa mkataba wake unafikia mwisho. ***(90min)***

#### SKRINIAR ANUKIA MADRID

REAL Madrid iko tayari kuipiku Tottenham Hotspur na kumsajili mlinzi wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

#### MELO KUREJEA LIVERPOOL

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp yupo tayari kumrudisha kiungo wa Brazil, Arthur Melo, mwenye umri wa miaka 26 kutoka Juventus ambako anacheza kwa mkopo. ***(Mirror)***

#### CAICEDO KUMFUATA POTTER

KIUNGO wa Brighton na Timu ya Taifa ya Ecuador mwenye umri wa miaka 19, Moises Caicedo, anapanga kumfuata kocha wake wa zamani, Graham Potter katika kikosi cha Chelsea. ***(Ole via Evening Standard)***

#### BELLINGHAM AGEUKA LULU

REAL Madrid na Chelsea zimejiunga na Liverpool na Manchester United katika mbio za kuwania saini ya kiungo, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund. ***(Sport)***

#### NUNES KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL inaweza kufufua mpango wake wa kutaka kumsajili kiungo wa Wolves na Timu ya Taifa ya Ureno, Matheus Nunes, 24. ***(UOL, via Mail)***

#### MESSI KUPEWA MKATABA

KLABU ya Paris St-Germain inataka fowadi wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, 35, na mlinzi wa Hispania, Sergio Ramos mwenye miaka 36 kusaini mikataba mipya. ***(AS)***

#### SOYUNCU KIMEELEWEKA

MLINZI wa Uturuki, Caglar Soyuncu, 26, ataondoka Leicester City na kujiunga na Atletico Madrid akiwa mchezaji huru kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(Mundo Deportivo )***

#### MOURINHO AMTAKA CHALOBAH

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Timu ya Taifa ya England, Trevoh Chalobah, 23, kutoka Chelsea ifikapo Januari. ***(Sport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RAPHINHA: NILIPOTEZA MARAFIKI KWA UHALIFU

**BARCELONA,** Hispania

**Asikitika kuona wachezaji wengine bora zaidi yake walipotea kwa sababu ya...**

WINGA wa Barcelona, Raphinha amekiri kuwa na marafiki wa utotoni, ambao baadhi yao walikuwa 'bora mara 10' kuliko yeye uwanjani wakimezwa na uhalifu ni mojawapo ya mambo muhimu yaliyomfanya ajikite zaidi kwenye soka.

**Raphinha, ambaye alikulia katika Wilaya ya Restinga, Porto Alegre amezungumza waziwazi kuhusu marafiki 'kupotea' kwa ulanguzi wa dawa za kulevya na uhalifu mwingine.**

Mbrazil huyo, aliyesajiliwa kwa euro milioni 68 na Barcelona majira ya joto baada ya miaka miwili ya kuvutia katika Ligi Kuu England akiwa na Leeds United, pia ameishukuru familia yake kwa kuhakikisha hakuacha shule au kuongozwa kwenye njia mbaya.

"Kwa mtu aliyezaliwa katika mtaa wa kihalifu kama mimi, ni vigumu kubaki makini. Ninatoka Restinga. Ni vigumu kufuata njia yako na kutopotea," alisema Raphinga akiiambia UOL Esporte.

"Fursa zinaonekana, na kuna nyingi. Wanaahidi njia rahisi ya kupata fedha. Na hapo ndipo watu hupotea. Nilikuwa shahidi, nilitembea pamoja na watu waliokuwa wakipotea.

"Nilipoteza marafiki wengi katika ulimwengu wa uhalifu, katika biashara ya dawa za kulevya...marafiki ambao walikuwa wachezaji bora mara kumi kuliko mimi na ambao wangeweza kuwa kwenye klabu kubwa ya soka duniani."

Aliendelea: "Kuwa na mifano hii karibu lilikuwa jambo muhimu katika kuweka mtazamo wangu. Nilijua nilichokitaka tangu nikiwa mdogo sana, kuwa mwanasoka.

"Sikukengeuka. Ikiwa leo wanazungumzia 'uchawi' wangu katika soka, nasema...huu ndio uchawi halisi. Ni shukrani kwa familia yangu, sikuacha shule na kupuuza fursa nilizopata."

Raphinha, aliongeza ilikuwa 'ndoto ya utotoni' kwake kucheza Barcelona, kwani alivutiwa sana na Ronaldinho - ambaye wanatoka wote mji wa Porto Alegre.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
BRENTFORD
VERSUS
ARSENAL
1 | 3.93
X | 3.60
2 | 1.82

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BALOTELLI ATETEWA KWA KULEWA



**SION,** Uswisi

MARIO Balotelli ameahidiwa kuungwa mkono kikamilifu na klabu yake ya FC Sion baada ya video ya mshambuliaji huyo wa Italia kusambaa katika mitandao ya kijamii usiku wa kuamkia jana akionekana kalewa sana.

Video hiyo iliyosemekana kurekodiwa Jumamosi mjini Lausanne, inamwonyesha Balotelli akitembea barabarani huku akiyumba.

Anaonekana ameongozana na mwanamke na mwanamume upande wake wa kulia, na ni kama walikuwa wakimkokota.

Balotelli hajazungumza lolote kuhusu video hiyo, lakini Sion imesisitiza kwa vyovyote vile haipingi wachezaji kwenda kusherehekea hasa baada ya kutoka kupata ushindi dhidi ya St. Gallen.

Taarifa ya klabu hiyo ilisema; “Tutamuunga mkono Balotelli kwa namna yoyote kwa sababu hakuna kosa alilolifanya. “Baada ya ushindi huo mkubwa wiki iliyopita, sehemu kubwa ya timu ilienda katika mji mkuu wa Vaud (Lausanne) kusherehekea mafanikio haya,” iliongeza taarifa ya Sion.

“FC Sion inasikitika kuwa video hii imechukua viwango visivyo vya lazima na visivyo na uwiano, jambo ambalo linadhuru sura ya mshambuliaji wetu.

“Klabu inachukua fursa hapa kukumbuka kwamba ina furaha sana na mwenendo wa sasa wa timu tangu kuwasili kwa Mario Balotelli.”



# Lukaku atemwa Ubelgiji

**BRUSSELS,** Ubelgiji

ROBERTO Martinez anatarajia Romelu Lukaku kurejea kwenye mazoezi ya Inter wiki ijayo, lakini amemuacha nje ya kikosi cha Ubelgiji kwa ajili ya mechi zijazo za Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Lukaku alipata jeraha la paja akiwa mazoezini mwishoni mwa mwezi uliopita, na kumfanya kukosa mechi dhidi ya AC Milan na mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich na Viktoria Plzen.

Mshambuliaji huyo, ambaye ni mfungaji bora wa Ubelgiji akiwa na mabao 68 katika mechi 102, pia anaonekana kuwa na shaka kwa mechi ya Nerazzurri ya Serie A dhidi ya Udinese ya leo na kumfanya Martinez kuchukua hatua kwa tahadhari na kumwacha kwa ajili ya mechi dhidi ya Wales na Uholanzi.

“Romelu anafanya maendeleo mazuri, ahueni yake inakwenda katika mwelekeo sahihi,” alisema Martinez.

“Kwa Romelu ilikuwa muhimu kutojiweka hatarini, kwa sababu kurudi tena kwa jeraha la aina hii itakuwa hatari sana kuelekea Kombe la Dunia.”

## HABARI MICHEZO

Y | CHEZA USHINDE KASINO

# SIMBA QUEENS KAMBINI KUELEKEA FAINALI ZA CAF

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba Queens kinatarajia kuingia kambini kesho kwa ajili ya kuanza maandalizi kuelekea Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake zinazotarajia kufanyika kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba 13, mwaka huu nchini, Morocco.

**Simba Queens, wamepata tiketi ya kushiriki mashindano hayo baada ya kutwaa ubingwa wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).**

Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, aliliambia gazeti hili jana baada ya kuwapa wachezaji mapumziko wa muda mfupi, sasa wataanza rasmi mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea fainali hizo ambapo wamepania kwenda kupeperusha vyema bendera ya CECAFA.

Makanya alisema wanatarajia fainali hizo zitakuwa ngumu na zenye ushindani, hivyo wanahitaji kujiimarisha na kuendelea kuimarisha kikosi kwa kusajili wachezaji wapya wawili kwa ajili ya kuongeza nguvu.

"Tutaingia kambini Jumatatu kujiandaa na Ligi ya Mabingwa, lakini baadaye tukimaliza huko Ligi ya Tanzania Bara itakuwa imeshaanza. Tulikuwa katika mapumziko, wachezaji wa nje wameanza kurejea nchini, pia tunatarajia kuongeza nguvu kwa kusajili beki mmoja wa kati na straika," alisema Makanya.

Simba Queens, ilitawazwa mabingwa wa CECAFA, baada ya kuifunga She Corporate kutoka Uganda bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa Agosti 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Katika fainali za Afrika, Simba Queens imepangwa Kundi A pamoja na timu za Asfar ya Morocco, Green Buffaloes ya Zambia na Determine Girls ya Liberia.

Kundi B linaundwa na Mamelodi Sundowns Queens ya Afrika Kusini, Bayelsa Queens (Nigeria), Wadi Degla (Misri) na TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).




Diwani wa Kata ya Kivukoni, Dar es Salaam, Sharik Choughule (wa pili kushoto), akimkabidhi nahodha wa timu ya soka ya vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), wa kata hiyo, Ali Songoro, vifaa vya michezo vilivyotolewa na ofisi ya diwani juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mlandege, Malindi hapatoshi Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mlandege imetamba imejiandaa vizuri kwa ajili ya kupata ushindi dhidi ya wapinzani wao, Malindi SC katika mchezo wa raundi ya tatu ya Ligi Kuu Zanzibar utakaochezwa leo kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Amaan.

Mlandege na Malindi ni 'dabi' ya miaka mingi katika ligi hiyo ya juu Zanzibar ingawa siku hizi umaarufu wake umepungua ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Kocha wa Mlandege FC, Abdallah Mohamed 'Bares' alisema ana matumaini makubwa ya kupata alama tatu katika mchezo huo ambao utawakutanisha 'mafahari wawili' wa muda mrefu.

Bares alisema, kikosi chake kimepanga mikakati mbalimbali kuhakikisha wanawafunga wapizani wao licha ya kucheza ugenini.

"Nashukuru kuelekea mchezo huo sina mchezaji ambaye amepata majeraha yatakayomfanya asiwepo kikosini, kila mmoja yuko tayari kupambana ili kuzipata alama tatu, mchezo utakuwa mgumu, wapinzani wetu wamejiandaa kuhakikisha hawapotezi lakini na sisi tumejiandaa kuhakikisha tunawapa raha mashabiki wetu," alisema Bares.

Naye Kocha Msaidizi wa Malindi, Ali Kisaka, alisema kikosi chake kimejiandaa kuhakikisha wanawaadhibu wapinzani wao katika mchezo huo muhimu.

"Malengo yetu ni makubwa mno japo ni mapema kuweka wazi, kila mchezo ambao upo mbele yetu sisi tunahesabu za kupata alama tatu muhimu, kila upande umejipanga," alisema kocha huyo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 18/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3326 | Udinese vs Inter | 3.65 | 3.65 | 1.88 |
| 14:00 | 2364 | St Mirren vs Celtic | 13.10 | 6.65 | 1.18 |
| 14:00 | 2623 | Brentford vs Arsenal | 3.93 | 3.60 | 1.82 |
| 14:00 | 5484 | Reims vs Monaco | 3.06 | 3.41 | 2.20 |
| 14:30 | 2242 | Racing Genk vs KAA Gent | 2.17 | 3.47 | 3.07 |
| 15:00 | 4791 | Osasuna vs Getafe | 1.78 | 3.28 | 4.95 |
| 15:00 | 5520 | Randers vs Silkeborg | 2.49 | 3.45 | 2.60 |
| 15:30 | 4656 | PSV Eindhoven vs Feyenoord | 1.84 | 3.85 | 3.60 |
| 15:30 | 5950 | Heerenveen vs Twente | 2.80 | 3.25 | 2.41 |
| 16:00 | 1206 | Clermont Foot vs Troyes | 2.25 | 3.27 | 3.07 |
| 16:00 | 1308 | Brest vs AC Ajaccio | 2.04 | 3.21 | 3.66 |
| 16:00 | 1678 | Kagera Sugar vs Dodoma FC | 2.46 | 2.66 | 3.15 |
| 16:00 | 2981 | Nice vs Angers | 1.62 | 3.87 | 5.03 |
| 16:00 | 3009 | Monza vs Juventus | 3.95 | 3.38 | 1.88 |
| 16:00 | 4648 | Marseille vs Rennes | 2.03 | 3.51 | 3.36 |
| 16:00 | 4910 | Cremonese vs Lazio | 4.01 | 3.76 | 1.77 |
| 16:00 | 5207 | Mamelodi Sundowns vs Amazulu | 1.55 | 3.65 | 6.20 |
| 16:00 | 5328 | Fiorentina vs Verona | 1.73 | 3.74 | 4.29 |
| 16:15 | 3050 | Everton vs West Ham | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 16:30 | 5513 | Union Berlin vs VfL Wolfsburg | 1.97 | 3.40 | 3.60 |
| 17:00 | 3758 | Basaksehir vs Fatih Karagumruk | 1.53 | 4.12 | 5.63 |
| 17:00 | 5627 | Motherwell vs Hearts | 2.75 | 3.30 | 2.44 |
| 17:00 | 5960 | Bragantino SP vs Goias | 1.52 | 3.73 | 5.70 |
| 17:15 | 3982 | Villarreal vs Sevilla FC | 1.73 | 3.69 | 4.55 |
| 17:45 | 4344 | AZ Alkmaar vs Ajax | 4.30 | 4.10 | 1.66 |
| 18:00 | 1160 | RB Salzburg vs Rapid Vienna | 1.29 | 5.32 | 7.29 |
| 18:00 | 3994 | Red Star Belgrade vs FK Napredak | 1.15 | 6.88 | 11.79 |
| 18:05 | 5275 | Nantes vs Lens | 3.00 | 3.40 | 2.23 |
| 18:30 | 2481 | Richards Bay FC vs TS Galaxy FC | 2.19 | 2.84 | 3.69 |
| 18:30 | 5089 | VfL Bochum vs FC Koln | 3.00 | 3.50 | 2.17 |
| 18:30 | 5360 | Djurgardens IF vs IFK Goteborg | 1.53 | 4.02 | 5.09 |
| 19:00 | 1114 | Roma vs Atalanta | 2.04 | 3.45 | 3.35 |
| 19:00 | 2703 | Derry City vs Shamrock Rovers | 2.33 | 3.14 | 2.85 |
| 19:00 | 3976 | Midtjylland vs Copenhagen | 2.27 | 3.43 | 2.92 |
| 19:00 | 4251 | Rosenborg vs Lillestrom | 1.95 | 3.51 | 3.61 |
| 19:00 | 5561 | OFI Crete vs PAOK | 4.51 | 3.25 | 1.83 |
| 19:30 | 2035 | Standard Liege vs Brugge | 3.66 | 3.66 | 1.89 |
| 19:30 | 2526 | Real Sociedad vs Espanyol | 1.73 | 3.63 | 4.64 |
| 19:30 | 4040 | Betis vs Girona | 1.69 | 3.62 | 4.93 |
| 20:00 | 1371 | Fenerbahce vs Alanyaspor | 1.49 | 4.41 | 5.61 |
| 20:00 | 4498 | Benfica vs Maritimo | 1.12 | 8.05 | 18.11 |
| 20:00 | 4623 | Columbus Crew vs Portland Timbers | 1.81 | 3.83 | 4.08 |
| 20:30 | 3990 | Hoffenheim vs SC Freiburg | 2.13 | 3.61 | 3.01 |
| 21:45 | 4444 | AC Milan vs Napoli | 2.16 | 3.35 | 3.15 |
| 21:45 | 5442 | Lyon vs Paris St Germain | 4.20 | 4.30 | 1.66 |
| 22:00 | 3041 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 22:00 | 3685 | Ceara CE vs Sao Paulo | 2.22 | 2.94 | 3.24 |
| 22:00 | 5138 | Anderlecht vs Kortrijk | 1.34 | 5.02 | 7.84 |
| 22:00 | 5913 | Flamengo vs Fluminense | 1.67 | 3.53 | 4.61 |
| 22:30 | 4871 | Sporting Braga vs FC Vizela | 1.31 | 5.23 | 8.44 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Septemba 18, 2022

Nipashe





‘Nilipoteza marafiki kwa uhalifu’ UKURASA 21



Mashabiki wa Simba wakicheza ngoma katika eneo la Mbagala, Dar es Salaam jana kwa ajili ya kuhamasisha wapenzi wa timu hiyo kujitokeza kuishangilia katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Nyasa Big Bullets itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga yatoboa siri

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amesema kiu ya mafanikio waliyonayo wachezaji, viongozi na mashabiki wa timu hiyo ndio sababu pekee inayochangia kuwapa ushindi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wanayoshiriki.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ndio vinara wa ligi hiyo na walianza vyema mashindano ya Ligi ya Mabingwa walipoikabili Zalan FC kutoka Sudan Kusini, ikiwafunga mabao 4-0 katika mechi ya kwanza na jana usiku walicheza mchezo wa marudiano.

Nabi aliliambia gazeti hili, wachezaji wanajituma sana mazoezini kwa ajili ya kupata namba lakini wanafahamu matokeo bora ndio yanawajenga na kulinda heshima ya klabu.

Kocha huyo alisema hali hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa kupata ushindi katika kila mechi wanayocheza na anaamini msimu huu watafika mbali katika michuano ya kimataifa.

“Kila mechi tunayocheza si rahisi, tunapambana ilia kusaka ushindi, ili uwe bingwa ni lazima utafute pointi, ushindi ni muhimu, lakini kupoteza pointi ni hatari, ninaamini kwa juhudi hizi, tutaendelea kuilinda heshima ya klabu na sisi wenyewe,” Nabi alisema.

Baada ya mechi ya jana, Yanga itasafiri kuelekea Mbarali, Mbeya kuifuata Ihefu katika mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Septemba 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Highland Estates mkoani humo.

# Simba, Big Bullets hapatoshi

## Mnyama afunguka hatamdharau mpinzani, Kipanga ya Zanzibar yatakata...

**Na Saada Akida**

KAZI moja. Hayo ni maneno yanayosemwa na benchi la ufundi la Simba kuelekea mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Nyasa Big Bullets kutoka Malawi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Simba wamedhamiria kulinda ushindi wa mabao 2-0 walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa wiki iliyopita jijini Lilongwe, shukrani kwa wafungaji wake, Moses Phiri na nahodha, John Bocco.**

Licha ya ushindi huo na kucheza kwa kiwango cha juu ugenini, miamba hao wameweka wazi wamejipanga kushuka dimbani kwa tahadhari ili yasijirudie yaliyotokea msimu uliopita walipotolewa na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Akizungumza jijini jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema maandalizi yote muhimu kuelekea mchezo huo yamekamilika na kikubwa kilichobakia ni kuwaombea dua vijana waamke salama na hatimaye watimize wajibu wao.

Mgunda alisema ameipata historia ya mechi ya awali kwa sababu hakuwa sehemu ya kikosi hicho na kuyafanyia kazi makosa yaliyoonekana na sasa wamejiandaa kwenda kulinda ushindi walionao.

Kocha huyo alisema anafahamu bado mechi haijamalizika hivyo ni jukumu la kila mmoja ndani ya Simba kuongeza juhudi ili kuhakikisha wanapambana na hatimaye wanasonga mbele.

“Wachezaji wanafahamu hilo, wanaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri, Sadio Kanoute amerejea na yuko fiti kwa mchezo wa kesho (leo), mchezaji yoyote atakayepewa majukumu basi yuko tayari kutafuta ushindi.

“Matokeo mazuri sio ya mtu mmoja, muunganiko na ahadi walionipa wachezaji basi najua wako tayari kutimiza wajibu, na kwa uwezo na mapenzi ya Mungu, kheri itapatikana,” alisema Mgunda.

Aliongeza kiufundi watahakikisha wanafikia mikakati ya klabu ikiwamo kufika hatua ya nusu fainali jambo ambalo linafahamisha vyema na benchi la ufundi pamoja na wachezaji.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein ‘Zimbwe Jr’, alisema maandalizi yako vizuri na benchi la ufundi limemaliza kila kitu na kazi kubwa imebaki kwao kusaka ushindi.

“Mechi ya kwanza tulihamasishana sana tukapata matokeo lakini hatujaishia hapo, hamasa inaendelea kuhakikisha kila mechi ikiwamo mechi ya kesho (leo), tunapata matokeo ya ushindi,” alisema Zimbwe Jr.

Naye Kocha Mkuu wa Nyasa Big Bullets, Callisto Pasuwa, alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu dakika 45 za mchezo wa kwanza zimemalizika na sasa wamejipanga kwa ajili ya kutafuta ushindi katika dakika 45 ya mchezo wa pili.

Pasuwa alisema hali ya hewa iko vizuri na wanachoangalia zaidi ni kuhakikisha wanavunja mwiko wa Simba kutofungwa kwenye uwanja wao.

“Wachezaji wako tayari kutafuta matokeo mazuri, tunaimani tutapata matokeo mazuri, mchezo sa soka lolote linaweza kutokea, Simba wameweza kupata matokeo ugenini na sisi tunaweza kupata ushindi ugenini,” alisema kocha huyo.

Aliongeza mechi hiyo itakuwa na ushindani kutokana na ubora wa timu zote na wao wamefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo uliopita na watashuka dimbani kwa tahadhari ya kutafuta ushindi zaidi ya mabao 3-0.

***Wakati huo huo***, Kipanga FC ya Zanzibar imesonga mbele katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kuiondoa Al Hilal Wau ya Sudan Kusini kwa penalti 4-3.

Matokeo ya jumla ya timu hizo yalikuwa ni sare ya mabao 2-2.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042



9 770856 541002 >